TAARIFA YA

Vol.04

# UTEKELEZAJI

## WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KWA KIPINDI CHA KUANZIA NOVEMBER 2020 – 2022

JIMBO LA ILEMELA
MKOA WA MWANZA



***MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN***
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(Chief Hangaya)



**Mhe. Dkt. Angeline S.l. Mabula (Mb)**
Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Ardhi
Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MNEC)

Imetayarishwa: Ofisi ya Mbunge wa jimbo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela,1 Barabara ya Bomani, 33281 Buswelu ILEMELA, MWANZA



**Mhe. Dkt. Angeline S.l Mabula (Mb)**

Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Ardhi
Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MNEC)



**Ndugu Yusuph Ernest Bujiku**

Mwenyekiti wa CCM wilaya Ilemela



**Mhe. Renatus Mulunga**

Meya wa Manispaa ya Ilemela

## Umoja wetu, Ushindi wetu, kwa pamoja tunaweza

## #KAZI IENDELEE

# YALIYOMO


1.0 Utangulizi ....4
2.0 Eneo la utawala ....5
2.1 Eneo la utawala na mgawanyo wake ....5
2.1.1 Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ....6
2.2 Idadi ya watu ....7
2.2.1 Sensa ya watu na makazi 2022 ....8
3.0 Hali ya kisiasa ....9
3.1 Utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 2020 - 2025 ....9
3.2 Utekelezaji wa ahadi za viongozi mhe. Rais, makamu wa rais na mbunge.... 10
4.0 Taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali.... 11
5.0 Huduma za jamii ....15
5.1 Sekta ya elimu ....15
5.1.1 Elimu ya msingi ....15
5.2 Elimu ya sekondari .... 19
5.2.1 Uandikishaji kwa miaka 3 (2020 hadi 2022).... 20
5.2.2 Miundombinu ya elimu ya sekondari. 2022 .... 20
5.2.3 Ujenzi wa madarasa 97 fedha za uviko.... 20
5.2.4 Ujenzi wa shule mpya....21
5.3 Michango ya ofisi ya mbunge kuunga juhudi za wananchi ....26
6.0 Uwezeshaji wananchi Kiuchumi.... 30
7.0 Sekta ya maji ....31
7.1 Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ....31
7.4 Mradi wa usambazaji maji nyamuhongolo ....33
8.0 Sekta ya afya ....36
8.1 Hospitali ya wilaya ....36
9.0 Huduma za kiuchumi .... 45
9.1 Sekta ya ardhi .... 45
9.1.5 Faida za upangaji miji na upimaji viwanja.... 46
9.1.6 Utoaji wa hati miliki.... 48
10.0 Sekta ya nishati .... 49
11.0 Huduma za kijamii nje ya mfumo .... 49
12.0 Ziara na mikutano mbalimbali jimboni ....55
12.1 Ujenzi wa chama....55
13.0 Sekta ya barabara ....58
13.1 Mchango wa ofisi ya mbunge katika matenenezo ya barabara ....58
14.0 Sekta ya mifugo na uvuvi ....67
14.1 Ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupimia samaki.... 68
14.2 Upanuzi wa uwanja wa ndege.... 69
14.3 Mradi wa uboreshaji miji na majiji.... 69
15.0 Sekta ya kilimo .... 70
16.0 Miradi ya kimkakati ....71
16.1 Ujenzi wa kituo cha basi na malori nyamhongolo ....72
17.0 Kampeni za ccm ....74
18.0 Mikutano ya ccm taifa ....75
19.0 Mikutano ya kitaifa....77
20.0 Sekta ya michezo ....82
20.0 Sekta ya michezo ....82
21.0 Matumizi ya mfuko wa jimbo .... 89
22.0 Shukurani ....95
22.1 Hitimisho ....97

## 1.0 UTANGULIZI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai, na maongozi yake mema katika utendaji wa kazi za umma hadi kufikia utoaji taarifa ya utekelezaji wa ilani ya chama. Kwa moyo wa dhati kabisa ninamshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuisimamia Serikali kwa weledi mkubwa chini ya falsafa ya # KAZI IENDELEE #, hakika wana Ilemela tunaona matunda ya uthubutu wa Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani katika kuliongoza Taifa letu.

Kipekee kabisa nimshukuru Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jambhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri ili kumsaidia majukumu katika Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kazi ambayo ninaifanya kwa juhudi na maarifa yangu yote na ninamuomba mwenyezi Mungu anizidishie hekima yakutenda kazi yangu kwa weledi huku nikiwa na hofu ya Mungu.

Aidha ninakishukuru Chama changu cha mapinduzi (CCM), wanachama, viongozi na wananchi kwa ujumla kwa kunipa ridhaa ya kuwa mbunge na kwa ushirikiano wanaonipatia katika utumishi wangu. Vilevile, ushirikiano mkubwa ninaoupata toka kwa waheshimiwa Madiwani wakiongozwa na Mstahiki Meya, Mhe. Renatus Bahebe Mulunga, Katibu wa Mbunge Ndg. Kazungu Safari Idebe, waratibu wote wa ofisi ya mbunge za kanda Ndg. John Makorosho (Kanda ya Nyakato, Bi. Rebeca Yusuph (Kanda ya Bugogwa), Bi Fatuma Kaloli (Kanda ya Kirumba), Bi Julieth Peter (Kanda ya Buswelu) Bw. Mpunji Mbekeje mratibu wa miundombinu Jimboni, Bw Mohamed Mgalu na Abubakar Juma kwa pamoja wanafanya majukumu yangu kuwa mepesi, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaishukuru Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela inayoongozwa na Mhe. Mwl Hassan Elias Masala, Ofisi ya Mkurungenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela chini ya Mhandisi Eng. Modest Joseph Apolinary pamoja na watumishi wote katika ofisi zao kwa ushirikiano wao mkubwa wanao utoa katika utendaji wao ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya chama kwa ufanisi zaidi, kwa pamoja nasema asanteni sana. Mwisho lakini si kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa upendo wao na kwa kunitia moyo wakati wote hasa ninapokutana na changamoto katika kutimiza majukumu yangu.

## 2.0 ENEO LA UTAWALA

### 2.1 Eneo la utawala na mgawanyo wake

Jimbo la Ilemela ni mojawapo kati ya majimbo tisa (9) ya uchaguzi katika mkoa wa Mwanza, lipo katika wilaya ya Ilemela, lina ukubwa wa kilomita za mraba 1080.55 kati ya hizo kilomita za mraba 828.45 sawa na asilimia 76 ni eneo la maji, kilomita za mraba 252.10 sawa na asilimia 23.3 ni eneo la nchi kavu. Wilaya ina Tarafa 1 Kata 19, na Mitaa171, Matawi ya chama 125 na Jimbo1 la uchaguzi Mbunge wake ni Dkt. Angeline S.L Mabula



**Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ilemela akipokea tuzo toka kwa Mkuu wa wilaya ya ilemela Mh Hassan Masala**



**Jengo la utawala kwa muonekano wa juu na mbele, ujenzi unaendelea vizuri**



## 2.1.1 Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi

**Ibara ya 122 (l), na 55 (h) (iv)** Inaitaka Serikali, kuendeleza ujenzi wa majengo yatakayotumika kama ofisi, kwa taasisi za Serikali, ili kuboresha mazingira kazini na kuyafanya yawe bora na kutoa huduma bora kwa wananchi. Utekelezaji wa takwa hili umefanyika kikamilifu, hadi sasa jengo limefikia 85%, na zimetumia takribani **Tsh. 3,521,930,946.64,** na linatarajiwa kutumia **Tsh. 3,800,000,000.00** hadi kukamilika

## 2.2 Idadi ya watu

Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na Makazi ya Augusti, 2022, Wilaya ya Ilemela ina watu **509,687** kati yao wanaume ni **241,137 sawa na 47.3%** na wanawake ni **268,550 sawa 52.7%** aidha kuna kaya **127,507** zenye wastani ya watu **4** kwa kaya. Jedwali hapa chini linaonasha takwimu za watu kila kata ndani ya wilaya ya Ilemela kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2022.

**JEDWALI LINALOONESHA IDADI YA WATU KILA KATA, JINSI, IDADI YA KAYA NA WASTANI WA WATU KWA KILA KAYA WILAYA YA ILEMELA**

| S/no | Jina la Kata | Idadi ya watu | Wanaume | Wanawake | Idadi ya kaya | Size ya kaya |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Buswelu | 42,614 | 19,784 | 22,830 | 10,020 | 4.3 |
| 2 | Nyakato | 29,560 | 13,843 | 15,717 | 8,131 | 3.6 |
| 3 | Nyamanoro | 24,624 | 11,751 | 12,873 | 7,357 | 3.3 |
| 4 | Kirumba | 32,364 | 15,693 | 16,671 | 8,688 | 3.7 |
| 5 | Kitangiri | 23,642 | 11,172 | 12,470 | 6,547 | 3.6 |
| 6 | Pansiasi | 16,274 | 7,862 | 8,412 | 4,262 | 3.8 |
| 7 | Ilemela | 26,091 | 12,346 | 13,745 | 6,819 | 3.8 |
| 8 | Bugogwa | 35,633 | 17,303 | 18,330 | 7,866 | 4.5 |
| 9 | Sangabuye | 13,004 | 6,363 | 6,641 | 2,409 | 5.4 |
| 10 | Kayenze | 17,201 | 8,562 | 8,639 | 4,187 | 4.1 |
| 11 | Shibula | 25,429 | 12,223 | 13,206 | 5,333 | 4.8 |
| 12 | Kahama | 21,816 | 10,237 | 11,579 | 4,768 | 4.6 |
| 13 | Kiseke | 30,664 | 14,399 | 16,265 | 7,275 | 4.2 |
| 14 | Kawekamo | 26,670 | 12,421 | 14,249 | 6,966 | 3.8 |
| 15 | Ibungilo | 24,295 | 11,220 | 13,075 | 6,905 | 3.5 |
| 16 | Nyamhongolo | 29,277 | 13,782 | 15,495 | 6,463 | 4.5 |
| 17 | Mecco | 23,294 | 10,744 | 12,550 | 6,170 | 3.8 |
| 18 | Buzuruga | 25,338 | 11,942 | 13,396 | 6,550 | 3.9 |
| 19 | Nyasaka | 41,897 | 19,490 | 22,407 | 10,791 | 3.9 |
| | **Jumla** | **509,687** | **241,137** | **268,550** | **127,507** | **4.0** |

### 2.2.1 Sensa ya Watu na Makazi 2022

Mwaka 2022 ulikuwa ni mwaka wa sensa ya watu na makazi, zoezi lilokuwana lengo la kupata takwimu muhimu kwa maendeleo ya taifa letu. Katikakuhakikisha zoezi hili linafanikiwa ofisi ya mbunge iliandaa mafunzo maalumkwa baadhi ya makundi muhimu katika jamii yakiwa na lengo la kuwafunda umuhimu wa sense, kuwapatia mbinu watakazoenda kuzitumia katika kutoa hamasa kwa wanajamii wanaowaongoza na kuwazunguka. Jedwali hapa chini linaonesha matokeo ya sensa ya watu na makazi kwa Jimbo la Ilemela.Matokeo ya sensa yanaonesha kuna ongezeko la watu 166,686 ukilinganisha na idadi ya watu **343,001** kwa mujibu wa sensa wa watu ya mwaka 2012, 0ngezeko hili ni sawa na asilimia **48.5963**

### 2.2.2 Taarifa ya Utekelezaji wa zoezi la anwani za Makazi Manispaa ya Ilemela

Zoezi la Anwani za Makazi ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya **Mwaka 2020-2025** kwa kila mwananchi na Taasisi za Umma na Binafsi kuwa na Anwani za Makazi katika kuhakikisha huduma zinatolewa kwa urahisi na unafuu kwa wananchi.

1. Utekelezaji ulioanza mwezi **Februari 2023**, umehusisha utambuzi,uainishaji na utoaji wa majina ya barabara na njia kutoka kwa wananchi katika ngazi ya Mitaa na Kata,
2. Kuandika namba za nyumba/majengo na maeneo ya Taasisi kwa kutumia vifaa mbalimbali na kuweka vibao vya namba kwa baadhi ya nyumba,
3. Kuchukua na kuingiza taarifa za umiliki wa nyumba/majengo na maeneo ya huduma kwenye mfumo tumizi wa Anwani za Makazi (NaPA) na, Kuandika na kusimika nguzo za majina ya Barabara na Mitaa katika maeneo mbalimbali.






Hadi kufikia **tarehe 30/06/2023** jumla ya taarifa za nyumba na **majengo 135,410** zimeingizwa kwenye mfumo, ambapo majengo ni **150,385** yakiwemo maghorofa 996. Utekelezaji wa zoezi hili umegharimu jumla ya T**sh. 206,705,593.60** ambazo zimetolewa na Serikali Kuu, Halmashauri na Taasisi za Umma **(TARURA NA TANROAD)**. Aidha, Wananchi mbalimbali waliopewa majina wamesimika nguzo na mbawa za majina katika baadhi ya barabara.

Manufaa yaliyopatikana kupitia zoezi hili ni kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, kuimarisha ulinzi na usalama, Serikali kupanga mipango ya kimaendeleo, kuongeza ajira na mapato ya Serikali kwa kuwezesha wananchi kushiriki uchumi wa kidijitali, hivyo kuchangia ukuaji wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.
Naomba kuwasilisha.

## 3.0 HALI YA KISIASA

Kwa ujumla hali ya kisiasa ni shwari. Tunamshukuru sana Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa maridhiano waliyofikia na vyama vya upinzani, hali hii inaashiria Taifa kuendelea na hali ya Utulivu na Amani huku kila chama kikifanya shughuli za kisiasa bila kubughudhiwa. Mikutano ya hadhara iliyoruhusiwa kufanyika iwapo itatumika vizuri italeta tija kwa watanzania wote.

### 3.1 Utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 2020 - 2025

***Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 imeandikwa kwa kuzingatia mambo makuu yafuatayo:-***



1. Kuendelea kushika dola kwa kuwaongoza Watanzania kwa njia ya kidemokrasia.
2. Utekelezaji wa Ilani kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, na mwelekeo wa sera za CCM kwa lengo la kuendeleakuwatumikia wananchi.
3. Kuondoa umaskini wa kipato.
4. Kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.
5. Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.
6. Kuendelea kudumisha Amani, Ulinzi na Usalama wa maisha ya wananchi na mali zao.

### 3.2 Utekelezaji wa ahadi za Viongozi Mhe. Rais, Makamu wa Rais na Mbunge

Taarifa hii ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 2020 – 2025 ni ya kipindi cha miaka miwili kuanzia November 2020 mpakaDesemba 2022. Taarifa imegusa maeneo kadhaa katika utekelezaji wake. Mbali na mambo mahususi yaliyotajwa katika Ilani ya uchaguzi, taarifa imeongelea pia utekelezaji wa ahadi za viongozi akiwemo Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuri Rais wa awamu ya tano na Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa awamu ya sita wakati akiwa makamu wa Rais wa awamu ya tano walizozitoa wakati wa kampeni 2020. Aidha utekelezaji uliofanywa na Halmashauriya Manispaa ya Ilemela pamoja na Serikali kuu, pamoja na ahadi binafsi za mbunge utekelezaji wake umeanishwa.

Pamoja na maelekezo hayo ya msingi ya Ilani, ahadi zifuatazo katika kipindi cha kampeni za October 2020 zilitolewa kwa kuzingatia uhitaji na hali ya maeneo ndani ya Jimbo na ambazo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango kikubwa sana kama itakavyooneshwa katika kila sekta kwenye taarifa hii. Ahadi zilizotolewa ni kama ifuatayo:

1. Kuboresha miundombinu ya Elimu katika shule za msingi na sekondari kwa kuhakikisha madarasa na nyumba za walimu zinajengwa na kuanzisha shule mpya palipo na uhitaji wa kufanya hivyo na uboreshaji wa matumizi ya TEHAMA mashuleni.
2. Kuboresha mazingira katika vituo vya afya na Zahanati kwa kuimarisha miundombinu na kuanzishwa maeneo mengine ya huduma kwa kadri ya uhitaji hususani katika kata za pembezoni na Kisiwa cha Bezi kata ya Kayenze.
3. Kuimarisha, kusogeza huduma za maji hasa kwenye maeneo yenye ukosefu mkubwa wa maji kwa kushirikiana na MWAUWASA na wadau wengine.
4. Kuboresha miundombinu ya barabara kwa kufanya matengenezo katika barabara zilizopo na kufufua barabara za zamani na kuanzisha barabara mpya.
5. Kuendeleza michezo mbalimbali ikiwemo Jimbo cup, muziki, n.k ili kuibua vipaji kwa vijana.
6. Kuisimamia Halmashauri ya manispaa ya Ilemela katika kuhakikisha 10% ya mapato ya mwezi inatengwa kwa ajili ya kuwawezesha akina

Mama, Vijana, na Watu wenye Ulemavu (PWD's).

7. Kufatilia kwa ukaribu utekelezaji wa ahadi za Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania walizozitoa kwawananchi wa Jimbo la Ilemela.
8. Kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu wa Shule za Serikali za Msingi na Serikali kwa kuboresha hali za ofisi za walimu na kununua Samani za Ofisini palipo na uhitaji.

## 4.0 Taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali.

Katika kipindi cha miaka miwili utekelezaji wa ilani ya uchaguzi umefanyika kwa ufanisi mkubwa sana. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kiwango kikubwa kwa kushirikiana na wawakilishi wa wananchi ambao ni Wenyeviti wa serikali za Mitaa, Madiwani na Mbunge wa Jimbo, Halmashauri na Serikali kuu. Kazi za mbunge kwa mujibu wa taratibu ni mwakilishi wa wananchi, anasimamia serikali na kutunga sheria, pia ni kiungo kati serikali na wananchi anaowawakilisha. Pamoja na majukumu hayo Mbunge anaowajibu wakuhakikisha kuwa utekelezaji wa ilani unafanyika kwa weledi mkubwa, na fedha za serikali zinatumika vyema.

Pamoja na kwamba taarifa ya utekelezaji wa ilani ni ya kipindi cha **Novemba 2020 ha Desemba 2022**, taarifa ya mapokezi ya fedha imegusa kipindi cha miaka miwili ya utendaji wa **Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika utoaji pesa za miradi ya maendeleo Jimbo/Wilaya ya Ilemela. Hakika tunajivunia kuwa na Rais mwenye maono, menye kujali ustawi wa watu anaowaongoza kwa kuhakikisha huduma za jamii zinawafikia watanzania wote kwa wakati.

Kwa kipindi cha miaka miwili Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela hadi kufikia Marchi 2023 imepokea kiasi cha **Shilingi 46,089,606,519.60** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao;

1. Shilingi **13,792,319,791.44** kwa ajili ya Ujenzi wa Standi ya Mabasi na Maegesho ya Magari Nyamhongolo
2. Shilingi **4,140,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 207 katika shule 49 za Sekondari kwa fedha za Mpango wa Maendeleo (COVID 19) na Pochi ya Mama
3. Shilingi **4,006,640,803.46** kwa ajili ya walengwa (kaya maskini), na

miradi ya kupunguza umaskini.

4. Shilingi **3,589,774,000.00** kwa ajili ya Upimaji wa viwanja 3250 katika eneo la mradi Sangabuye
5. Shilingi **4,403,702,424.00** kwa ajili ya Elimu Bila Malipo (EBM) kwa shule za Sekondari
6. Shilingi **2,136,568,563.15** kwa ajili ya Elimu Bila Malipo (EBM) kwa shule za Msingi
7. Shilingi **1,750,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri
8. Shilingi **1,300,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi na ukamilishaji wa Hospitali ya Wilaya
9. Shilingi **500,000,000.00** kwa ajili Ujenzi wa kituo kipya cha afya cha Kayenze
10. Shilingi **470,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Buzuruga
11. Shilingi **150,000,000.00** kwa ajili ya Ukamilishaji wa Zahanati 3 (Masemele, Lumala, na Nyamadoke)
12. Shilingi **112,517,172.00** kwa ajili ya Ukamilishaji wa madarasa 9 katika shule za Msingi
13. Shilingi **300,000,000.00** kwa ajili ya Ukamilishaji wa maabara 10 katika shule za Sekondari
14. Shilingi **130,573,956.00** kwa ajili ya Ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya mialo
15. Shilingi **300,000,000.00** kwa ajili ya Ununuzi wa vifaa tiba katika Zahanati ya Nyamadoke, Masemele na Lumala na Kituo vya Afya Kayenze
16. Shilingi **144,157,000.00** za kuchochea Maendeleo (Mfuko wa Jimbo)
17. Shilingi **35,617,139.55** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kunawia mikono katika shule 2 za msingi na shule 1 ya sekondari.
18. Shilingi **150,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba 2 za 2 in 1 katika shule za msingi Isanzu na Hekima na maabara 1 katika shule ya sekondari Bwiru Wasichana
19. Shilingi **100,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa bweni 1 la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Buswelu
20. Shilingi **80,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa 4 katika shule za msingi Tumaini na Mkudi
21. Shilingi **55,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 na matundu

10 ya vyoo katika shule ya msingi Nyamanoro

22. Shilingi **20,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa bweni 1 Shule ya Sekondari Sangabuye

23. Aidha, shilingi **8,242,735,670.00** zimetolewa kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali ya Afya, Elimu, uvuzi, upimaji wa ardhi, maendeleo ya jamii, barabara, masoko na biashara.

| S/n | Sekta | Mapokezi ya fedha | Chanza cha fedha | Mradi uliotekelezwa | Malezo | Hatua iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2021/2022** | **2022/2023** | | | |
| 1 | Afya | 1,350,000,000 | | Serikali kuu/Tozo | Ujenzi hospital ya wilaya, zahanati (Masemele,Lumala na Nyamadoke), Kituo cha afya Kayenze | Miradi imekamilika |
| 2 | Afya | 267,282,590 | 229,974,548 | Mapato ya ndani | -Ujenzi wa wodi ya wazazi Buzuruga, Jengo la kujifungulia Nyakato, Jengo la kufulia na nyumba ya mtumishi kituo cha afya Karume na kuwezesha shughuli za lishe.<br>- Ukamilishaji wa zahanati ya Kawekamo,ujenzi wa wodi ya kinamama Buzuruga, matengenezo ktk kituo cha Buswelu, Karume na Hospital ya wilaya | Shughuli za lishe zimefanyika. Miradi imekamilika kasoro ujenzi wa wodi ya wazazi unaendelea |
| 3 | Afya | | 194,160,114 | TASAF | Ujenzi wa Zahanati na nyumba ya mtumishi mtaa wa Mihama | Ujenzi unaendelea |
| 4 | Afya | | 229,974,548 | Mapato ya ndani | | Ujenzi inaendelee |
| 5 | Elimu Sekondari | 1,940,000,000 | 2,200,000,000 | Serikali kuu/ Covid | Ujenzi vyumba 207 vya madarasa katika shule 26 za sekondari | Ujenzi umekamilika |
| | | 35,617,140 | | WASH | Ujenzi wa miundombinu ya kunawia Nyamanoro na Buswelu sekondari | Ujenzi umekamilika |
| | | 470,000,000 | | SEQUIP | Ujenzi wa shule mpya Buzuruga sekondari | Ujenzi umekalika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 308,596,989 | 217,351,705 | TASAF | Ujenzi wa shule mpya na hostel Igogwe Sekondari | Ujenzi umekamilika |
| | | 275,140,712 | 70,321,060 | Mapato ya ndani | - Ujenzi vyumba 17 vya madarasa, vyumba 2 vya maabara, Ofisi 3, Bweni 1 katika shule za Sekondari,<br>-Ununuzi wa vitanda bwiru wavulana, Mashimo ya vyoo Bujingwa sekondari | Mradi umekemilika |
| 6 | Elimu Msingi | 353,027,850 | | Mapato ya ndani | Ujenzi wa vyoo 15, ofisi 1 katika shule za msingi | Ujenzi umekamilika |
| | | 80,000,000 | | EP4R | Ujenzi madarasa 4 shule ya msingi Mkundi | Ujenzi umekamilika |
| | | 55,000,000 | | TEA | Ujenzi madarasa 2 na matundu 10 shule ya msingi Nyamanoro | Ujenzi umekamilika |
| 7 | Uvuvi | 130,573,956 | | Serikali kuu | Ujenzi wa Ofisi, Uzio,na banda la kupokelea samaki Mwalo wa Igombe na ujenzi wa ofisi na choo mwalo wa Kayenze | Ujenzi umekamilika |
| 8 | Utawala | 1,000,000,000<br>19,581,953,639 | | Serikali kuu | Jengo la utawala makao makuu.<br>Ujenzi kituo cha mabasi na maegesho ya malori | Ujenzi unaendelea<br>Mradi umekamilika |
| | | 532,209,447 | | Mapato ya ndani | Ununuzi wa magari 4 | Magari 2 yamefika 2 bado |
| 9 | Ardhi | 3,589,774,000 | | Serikali kuu | Mradi wa viwanja 3,500 Kata ya Sangabuye | Mradi umekamilika uuzaji viwanja unaendelea |
| | | 521,401,833 | | Mapato ya ndani | Fidia kwa wananchi waliopisha mradi | Fidia imelipwa |
| 10 | Ardhi | | 350,480,058 | Mapato ya ndani | Ulipaji fidia wananchi waliopisha ujenzi wa Sekondari ya Lumala na Nyasaka | Fidia imelipwa |
| 11 | Maendeleo ya jamii | 559,000,000 | 479,000,000 | Mapato ya ndani | Mikopo kwa vikundi vya Wanawake108, Vijana 31 na wenye ulemavu 7 | Mikopo imetolewa |
| 12 | Biashara na uwekezaji | 237,505,000 | | Mapato ya ndani | Uwezeshaji mradi wa Tofali | Mradi unaendelea |
| | | 84,007,765 | | | Ukarabati wa masoko | Mradi umekamilika |

## 5.0 HUDUMA ZA JAMII

### 5.1 Sekta ya Elimu

### 5.1.1 Elimu ya Msingi

Jimbo la Ilemela lina shule za msingi **129** kati ya hizo shule **76** ni sa serikali na shule **53** ni za taasisi binafisi zikiwemo shule zilizochini ya madhehebu ya dini. Idadi ya watoto wa shule ni kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba ni **86,679** kati yao Wasichana ni **44,375** na Wavulana **42,304 .**

Ibara ua 16 ya ilani ya uchaguzi imeitaka serikali kuimarishwa na kuendelezwakwa mifuko mbalimbali na programu, Maalum za kusaidia wananchi wenyekipato cha chini na wenye, Mahitaji maalum ili waweze kuondokana na umasikini. Lengo likiwa ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaohitimu darasa la sabana kufaulu wanaanza masomo yao kwa wakati nakatika mazingira rafikiKwa kipindi cha miaka miwili uboreshaji miundombinu shule za msingi, jumlaya shule mpya tano zimeanzishwa ambazo ni; **1) Shule ya msingi Buyombe Kata ya Kahama, 2) Shule ya Msingi Bujingwa Kata ya Buswelu, 3) Shuleya msingi Kangae kata ya Nyakato, 4) Shule ya msingi Kahama kata yaKahama na 5) Shule ya msingi Shibula kata ya Shibula**



**Shule ya msingi Shibula kata ya Shibula**

## Taarifa fupi ya maendeleo ya ujenzi wa miundombinu




**Aidha Mhe.Masala ametoa shukrani kwa benki ya NBC kwa niaba ya timu nzima ya Ilemela kwa kutimiza ahadi yao huku akiwaomba kuendelea kuunga juhudi mbalimbali za maendeleo hususan kuunga mkono zoezi la ujenzi wa vyumba vya madarasa linaloendelea kwa shule za msingi za Manispaa ya Ilemela.**

| s/n | Maelezo | Mahitaji | Halisi | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idadi ya waalimu | 1,745 | 1,469 | 276 |
| 2 | Vyumba vya madarasa | 1,762 | 654 | 1,108 |
| 3 | Idadi ya madawati | 2644 | 22575 | 3869 |
| 4 | Idadi ya nyumba za waa-limu | 1492 | 94 | 1398 |
| 5 | Matundu ya vyoo | 2,889 | 1,047 | 1,842 |

### (a) Ujenzi wa Miundombinu katika shule za Elimu ya msingi

Kwa kipindi kifupi sana chini ya uongozi thabiti wa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania shule mpya na miundombinu mingine imejegwa katika kata 6, ambayo ni ujenzi wa vyumba vya madarasa, Nyumba za waalimu na matundu ya vyoo kwa gharama ya **Shs 226,500,000/=**Fedha toka mapato ya ndani na Serikali kuu kama ifuatavyo;



**Madawati yaliyopo katika shule ya Msingi Kahama yaliyonunuliwa kutokana na Harambee ya wadau wa elimu iliyoandaliwa na Mkuu wa Wilaya Mbunge alichangia dawati 570**



**Nyumba ya mtumishi shule ya msingi Hekima**



**Nyumba wa walimu 2:1 shule ya msingi Isanzu**



**Shule mpya ya msingi Kangae picha ya juu ni vyumba vya madarasa, picha ya chini vyoo cha watoto wa shule**



| s/n | Kata/Shule | Miundo mbinu | Gharama | Hatua iliyopo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shibula/Nyamwilolelwa | Madarasa 2 | 40,000,000 | imekamilika |
| 2 | Bugogwa/Isanzu | Nyumba ya Mwalimu | 50,000,000 | Imekamilika |
| 3 | Ibungilo/Hekima | -do- | 50,000,000 | -do- |
| 4 | Nyakato/Kangae | Madarasa 5 | 54,000,000 | imekamilika |
| 5 | Kahama/Lukobe | Matundu vyoo 20 | 20,000,000 | Imekamilika |
| **Jumla** | | | **226,500,000** | |

(b) **Uandikishaji wanafunzi darasa la awali na msingi 2020/21 na 2021/22**

| s/n | Mwaka | Maoteo | Walioandikishwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2020 | 7,656 | 6,689 | 87 |
| 2 | 2021 | 7,455 | 5,404 | 72 |
| 3 | 2022 | 7,602 | 7,160 | 94 |
| **Jumla** | | **22,713** | **19,253** | **84** |

(c) **Uandikishaji wanafunzi darasa la Kwanza 2020/21 na 2021/22**

| s/n | Mwaka | Maoteo | Walioandikishwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2020 | 9,824 | 10,744 | 109 |
| 2 | 2021 | 10,082 | 10,557 | 105 |
| 3 | 2022 | 10,543 | 12,472 | 118 |
| **Jumla** | | **70,449** | **33,773** | **110.6** |

## 5.2 Elimu ya Sekondari

Ilani ya uchaguzi ilikuwa inaitaka serikali kujenga na kukarabati miundombinuya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na Kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **600** mwaka **2020** hadi **1000** ifikapo **2025.** Lengo ikiwa ni kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasakatika shule za sekondari na kuhakikisha

kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza anaanza masomo kwa wakati.

Jimbo la Ilemela lina jumla ya shule za sekondari **50** kati ya hizo shule **27** za serikali na shule **23** za binafsi. Kidato cha tano na sita tunazo shule **7** kati ya hizo shule **3** za serikali na **4** shule binafsi.

Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari ni **31,483** wasichana **16,365** na wavulana **15,118.**

### 5.2.1 Uandikishaji kwa miaka 3 (2020 hadi 2022)

| s/n | Mwaka uandikishaji | Waliochaguliwa | Walioripoti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2020 | 8,711 | 9,439 | 108 |
| 2 | 2021 | 9,869 | 9,146 | 93 |
| 3 | 2022 | 10,486 | 10,102 | 96 |
| **Jumla** | | **29,066** | **28,687** | **99** |

Uandikishaji wanafunzi wenye mahitaji maalum **2020** ni wanafunzi **10**, mwaka **2021** wanafunzi **29** na mwaka **2022** wanafunzi **25.**

### 5.2.2 Miundombinu ya elimu ya sekondari. 2022

| s/n | malizo | Mahitaji | Halisi | Pungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **Madarasa** | **700** | **584** | **116** | **16.57** |
| **2** | **Maabara** | **81** | **71** | **10** | **12** |
| **3** | **Samani** | **31,483** | **26,312** | **5,171** | **84** |
| **4** | **Waalimu** | **1384** | **193** | **291** | **21** |

### 5.2.3 Ujenzi wa madarasa 97 fedha za UVIKO

Ujenzi wa madarasa 97 katika shule za sekondari za Manispaa ya ilemela umekamilika. Mradi uligharimu jumla ya **Tsh.1,940,000,000.00** kutoka Serikali kuu kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya **UVIKO 19**. Katika kipindi cha **Novemba 2020** hadi **Desemba 2022** tumeendelea kushirikiana na wananchi, viongozi ngazi mbalimbali wa Chama na serikali katika kuongeza miundombinu ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa, maabara na ofisi za walimu katika Shule za msingi na Sekondari. Pamoja na uboreshaji wa miundombinu, jumla ya shule mpya 6 elimu ya sekondari na shule mpya **5** elimu ya

msingizimejengwa na kuondoa adha ya mbanano ama mlundikano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa, vilevile uboreshaji wa matumizi ya TEHAMA shuleni umefanyika katika baadhi ya za sekondari.

### 5.2.4 Ujenzi wa shule mpya

Utekelezaji wa kauli mbiu ya jimbo "ILEMELA NI YETU, TUSHIRIKIANEKUIJENGA" umekuwa ukifanyika kwa vitendo, aidha ushiriki wa pande zote tatu wananchi, Mbunge na Serikali, umeonekana wazi katika ujenzi washule kwa maana ya moja, wananchi wanaanzisha wazo na kuaza ujenzi wamsingi, ofisi ya Mbunge inatoa tofali ili kufanikisha ujenzi wa boma na mwishoHalmashauriama serikali kuu inakamilisha ujenzi. Shule mpya za Sekondari zilizojengwa ni pamoja na; 1) **Shule ya Sekondari Semba Kata ya Shibula,**

**2) Sekondari ya Lubuka Kata ya Kahama, 3) Sekondari ya Igogwe Kata ya Bugogwa, 4) Sekondari ya Buzuruga Kata ya Buzuruga, 5) Sekondari ya Semba Kata ya Shibula na 6) Sekondari ya Nyamhongolo Kata ya Nyamhongolo**, shule zote zimeanza kutumika hivyo kupunguza usumbufuwa kutembea umbali mrefu kwa watoto na pia kuondoa msongamano katikavyumba vya madarasa.





Shule mpya ya Sekondari ya Buzuruga imeanza kutumika pamoja na kuwa ujenzi wa baadhi ya miundombinu unaendelea



Ujenzi wa Vyumba vya madarasa Shule mpya ya Sekondari Igogwe kwa Fedha za TASAF



Shule mpya ya Sekondari ya Masanza kata ya Kahama



Shule mpya ya sekondary ya Nyamhongolo, ujenzi wa miundombinu unaendele

### 5.2.5 Miradi inayotekelezwa kwa fedha za tasaf pamoja na michango ya wananchi, mbunge na halmashauri ya manispaa.

Tunamshukuru sana Mh Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuletea **jumla ya Shs. 703,757,592.55** ikiwa ni fedha za miradi na usimamizi. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na;

| Na. | Kata | Mradi | Pesa ya mradi iliyopokelewa nausimamizi |
|---|---|---|---|
| 1 | Bugogwa | Ujenzi wa vyumba vinne vyamadarasa na kuweka samani | 128,373,351.74 |
| | | Ujenzi wa jengo la utawala | 115,005,938.88 |
| | | Ujenzi wa Maabara ya sayansi | 65,190,698.62 |
| 2 | Kitangiri | Ujenzi wa zahanati (OPD)Mihama | 92,779,762.49 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi,jengo la ukunga na vyoo matundu manne ya vyoo - Mihama | 94,586,779.06 |
| 3 | Bugogwa | Ujenzi wa hostel | 142,630,366.16 |
| | | Ujenzi wa Maabara ya sayansi | 65,190,698.62 |
| **Jumla** | | | **703,757,592.55** |



**Shule mpya ya sekondari ya Igogwe, inajengwa kwa fedha za TASAF, michango ya wananchi na Mbunge, ujenzi unaendelea**

Ujenzi wa shule mpya ya sekondari Igogwe mpaka sasa umegharimu kiasi cha **Tsh.308,569,989.22** fedha kutoka mfuko wa kunusuru Kaya maskini (TASAF) ujenziupo katika hatua za mwisho za umaliziaji lakini tayari wanafunzi waposhuleni kutokana na uhitaji mkubwa wa shule katika eneo hilo. Lengo la ujenziwa shule hiyo ni kuongeza shule mpya katika kata zenye idadi kubwa ya wanafunzi. Ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.



**Kwa juu jengo la Maabara limekamilika na chini chumba cha Maabara shule ya sekondari ya Bwiru wasichana**



## 5.3 Michango ya ofisi ya mbunge kuunga juhudi za wananchi

### 5.3.1 Hali ya miundombinu

Kumekuwepo na uhitaji mkubwa wa miundombinu katika sekta ya elimu kutokanana ongezeko la idadi ya wanafunzi kila mwaka. Kutokana na changamoto hiyo, ofisi ya Mbunge kwa kushirikiana na Wananchi, Ofisiya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Serikali Kuukwa usimamizi mkubwa na mzuri unaofanywa na Ofisi ya Mkuu wa Wilayaya Ilemela Mhe. Mwl. Hassan Elias Masala, kazi kubwa imefanyika kuziba mapungufu ya miundombinu hususani kabla ya fedha za Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kutolewa kwaajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ikiwemosuala la vifaa vya ujenzi, madawati, samani katika ofisi za waalimu kupitia fedha za mfuko wa jimbo na fedha binafsi za mbunge, wadau na taasisi ya Angeline Foundation.

### 5.3.2 Ugawaji wa vifaa vya ujenzi (Tofali na Saruji)

Katika kipindi kinacho tolewa taarifa, shughuli za kimaendeleo zifuatazo kwa zimefanyika kupitia ofisi ya Mbunge kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za wananchi. **Jumla ya mifuko 2,990 ya saruji** imetolewa kwa ajili ya kuchangia shughuli za ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya. Idadi ya **tofali 102,185** zilitengenezwa na kugawiwa katika kata mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari pamoja na zahanati wilayani. **Tarehe 20 August,2022** ilifanyika ziara yenye lengo la kukagua usambazaji wa vifaa hivyo katika kata mbalimbali jimboni kujiridhisha kama vifaa husika viliwafikia walengwa katika Shule za Msingi, Sekondari na zahanati zilizokuwa katika hatua za ujenzi. Maeneo yaliyopata mgao huo ni kama ifuatavyo;

**Mchanganuo wa mgao wa vifaa vya ujenzi**

| NA | MCHANGO | MAHALI | THAMANI |
|---|---|---|---:|
| 1 | Saruji mifuko 2,200 | Ilemela Manispaa | 94,782,000 |
| 2 | Saruji mifuko 580 | Ilemela Manispaa | 27,840,000 |
| 3 | Saruji mifuko 50 | Kilimani Sekondari | 1,125,000 |
| 4 | Saruji mifuko 50 | Nyamhongolo Sec | 1,125,000 |
| 5 | Saruji mifuko 50 | Nyasaka Sekondari | 1,125,000 |
| 6 | Saruji mifuko 50 | Kangaye Sekondari | 1,125,000 |
| 7 | Saruji mifuko 10 | Pasiansi Sekondari | 200,000 |
| | **Jumla:** | | **127,322,000** |

### 5.3.3 Ununuzi wa Madawati

Katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Desemba 2022 tumefanikiwa kutengeneza na kugawa madawati **570 yenye thamani ya shilingi 39,900,000/=** ambazo ziligawiwa katika Shule zilizokuwa na uhaba mkubwa. Nimshukuru sana Mhe Mwl Hassan Masala mkuu wa wilaya pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa kwa ubunifu na uthubutu wa kuandaa chakula cha hisani kwa ajili ya kuchangia madawati kwa shule za msingi amba ofisi ya mbunge ilishiriki vizuri kwa kushirikiana na wadau wengine walioshiriki katika uchangiaji wa madawati.

### 5.3.4 Ununuzi wa Samani za Ofisi za Walimu

Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa 2020 moja ya ahadi za mgombea ilikuwa ni kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa walimu wa shule za sekondari zote jimboni. Ahadi hiyo imeitekelezwa kwa **60%** kwa shule zote zikiwemo na baadhi ya shule za msingi. Samani za ofisini zenye gharama ya**shilingi milioni Tsh 36,000,000/=** zilinunuliwa na kusambazwa katika ofisi za walimu zenye uhitaji mkubwa na zoezi hili ni endelevu kwa kadili bajeti ya ofisiyangu itakavyokuwa ikiruhusu.

| Na | Mchango | Mahali | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1 | Ununuzi wa Samani (Sec) | Kata ya Nyamanoro | 2,000,000.00 |
| 2 | Ununuzi wa Samani (Sec) | Kata ya kitangiri | 2,000,000.00 |
| 3 | Ununuzi wa Samani (Sec) | Kata ya Mecco | 2,000,000.00 |
| 4 | Ununuzi wa Samani (Sec) | Kata ya Kirumba | 3,000,000.00 |
| 5 | Ununuzi wa Samani (Sec) | Kata 15 za awamu II | 27,000,000.00 |
| | **Jumla** | | **36,000,000.00** |

### 5.3.5 Uboreshaji wa Tehama Mashuleni

Katika kuendana na mabadiliko ya kisayansi ulimwenguni ambayo yamekuwa yakisisitizwa matumizi ya Tehama, nikiwa mtumishi wa wana Ilemela nimeen- delea kusimamia matumizi ya kompyuta mashuleni kwa ajili ya kujifunzia.Katika awamu ya kwanza ya uwakilishi wa mbunge wangu 2015/2020 nifan-ikiwa kununua na kugawa seti za **kompyuta 20** zenye thamani ya **Shilingi 30,000,000/=** Katika kipindi tunachokitolea

taarifa ofisi ya mbunge imeende-lea na ugawaji wa kompyuta mashuleni kwa kugawa seti saba za komputer**. Komputer 4 shule ya sekondari Kabuhoro na komputer 3** katika idara ya elimu ya halmashauri ya manispaa ya Ilemela**.**

### 5.3.6 Mchango Katika shule mpya za sekondar.

Ili kurahisisha shughuli ya uboreshaji miundombinu katika shule za sekondarina msingi, ofisi ya mbunge iliendelea kuchangia vifaa vya ujenzi kwa kutoa to-fari ili kuunga mkono nguvu za wananchi katika uboreshaji wa miundombinuya elimu. Shule zote mpya zilizojengwa, tofali zilitolewa na ofisi ya mbunge ili kusimamisha maboma ya vyumba vya madarasa katika ujenzi wa shule mpyakama inavyoonesha hapa chini;

### 5.3.7 Mchanganuo wa mgao wa tofali kwenye shule mpya

Aidha **Shule mpya ya Sekondari la Buzuruga** imejengwa kwa fedha toka Serikali Kuu ambapo Mh Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri yaMuungano wa Tanzania aliitikia na kujibu kilio cha wananchi wa Buzuruga.**Kata hii ilikuwa chini ya upinzani kwa miaka 15 kuanzaia 2005 hadi 2020** na haikuwahi kuwa na shule ya Sekondari hata moja, ikiwa chini ya uongozi wa upinzani mpaka mwaka 2020 ilipochukuliwa na Chama Cha Mapinduzi.Serikali ilitoa Shilingi milioni mia nne na sabini **Tsh. 470,000,000/=** kwa ajiliya **ujenzi wa vyumba vya madarasa nane, maabara tatu, jengo la utawala, Jengo la Tehama moja matundu 20 ya vyoo** na vyote vimekamilika na shuleimepokea watoto wa kidato Januari, 2023

**Shule ya Sekondari Igogwe** ipo Kata ya Bugogwa. Ujenzi wa Shule hii pia ulianzishwa na wananchi kupitia Vikao vya mitaa na Kata, Ofisi ya Mbunge ilishiriki na Ofisi ya Mkurugenzi alikamilisha na tayari imepokea watoto 160 kati ya 167 waliotakiwa kuriport Januari, 2023. Pia tunashukuru Serikali ya awamu ya sita kupitia mfuko wa kunusuru kaya maskini – TASAF jumla ya fedha **Tsh 308,569,989.22** zilitolewa kwa ajili ya **ujenzi wa madarasa, maktaba, nyumba ya walimu, na jengo la utawala.**

**Shule ya sekondari Kabusungu** shule mpya ipo kata ya Sangabuye inajengwakwa juhudi za wananchi na Halmashauri ya Manispaa watafanya umaliziaji baada ya maboma kuwa yamesimama. Ujenzi unaendelea na ofisi ya Mbungeimeshakabidhi **tofali 3,600** yenye jumla ya **Tshs 4,320,000/=** kwa ajili ya ujenzi awamu ya kwanza.

| S/n | Jina la shule | Idadi ya tofali | Thamani | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sekondari ya Semba | 8,500 | 10,200,000.00 | Shule inatumika |
| 2 | Sekondari ya Ma-sanza | 9,700 | 11,640,000.00 | Shule inatumika |
| 3 | Sekondari ya Igogwe | 7,600 | 9,120,000.00 | Shule inatumika |
| 4 | Sekondari ya Ka-busungu | 3,600 | 4,320,000.00 | Ujenzi unaendelea |
| | **Jumla** | **29,400** | **35,280,000.00** | |

| S/ NO | MIUNDOMBINU | IDADI 2015 | IDADI 2021/ 2022 | ONGEZEKO 2015 – 2022 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyumba vya Maadarasa | 320 | 485 | 165 |
| 2 | Matundu ya vyoo | 286 | 422 | 136 |
| 3 | Meza | 14,726 | 23,216 | 8,490 |
| 4 | Viti | 14,726 | 23,216 | 8490 |
| 5 | Vyumba vya maabara | 59 | 77 | 18 |
| 6 | Nyumba za walimu | 86 | 87 | 1 |

### 5.3.8 Utengenezaji Madawati

Katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Disemba 2022 tumefanikiwa kutengeneza madawati 120 na kuyagawa kwa Shule 4 za msingi ambazo hazikupata mgawo wa madawati yaliyotengenezwa kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa ujumla hali ya miundombinu katika shule za msingi si ya kurudhisha sana, upungufu ni mkubwa zaidi hivyo tunalo jukumu kubwa la kushirikisha wadau wa elimu ili kukwamua.

| Na | Mchango | Mahali | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1 | Madawati 30 | Chasubi S/M | 2,250,000/= |
| 2 | Madawati 30 | Pasiansi S/M | 2,250,000/= |
| 3 | Madawati 30 | Igombe S/M | 2,250,000/= |
| 4 | Madawati 30 | Nyamadoke S/M | 2,250,000/= |
| **Jumla:** | | | **9,000,000/=** |

Halmashauri kwa kutumia mapato ya ndani ilifanikiwa kujenga vyumba 33 vya madarasa, kutengeneza dawati 1,100 na ofisi 3 za walimu. Pamoja na jitihada hizo bado kuna changamoto ya miundombinu katika shule za msingi.

## 6.0 Uwezeshaji wananchi Kiuchumi

### 6.1 Uwezeshaji vikundi vya Jamii, Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu

Kusudio la uwakilishi ni kuisimamia Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika kuhakikisha 10% ya mapato ya mwezi inatengwa kwa ajili ya kuwawezesha akina Mama, Vijana, na Watu wenye Ulemavu (PWD's). Natambua awali hapakuwa na sheria iliyokuwa inazilazimisha Halmashauri kutenga 10% huivyo wakurugenzi walikuwa wanaamua tu watenge kiasi gani kwa utashi, jambo ambalo kwasasa sheria inawalazimisha kutenga fedha hizo kila mwezi kutoka mapato ya ndani.

| Mwaka | Mapato ya ndani | Revolvingfund | Wanawake | Vijana | Wenye ulemavu | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kiasi | Idadi | Kiasi | Idadi | Kiasi | Idadi |
| 2020/21 | 385,115,000 | 553,700,000 | 632,925,000 | 154 | 278,890,000 | 51 | 27,000,000 | 11 |
| 2021/22 | 555,000,000 | 91,598,000 | 380,000,000 | 73 | 247,598,000 | 23 | 19,000,000 | 6 |
| 2022/23 | 479,000,000 | 163,100,000 | 402,000,000 | 49 | 226,000,000 | 13 | 14,000,000 | 4 |
| **Jumla** | **1,419,115,000** | **808,398,000** | **1,414,925,000** | **276** | **752,488,000** | **87** | **60,100,000** | **21** |

## 7.0 SEKTA YA MAJI

Ibara ya 100 ya ilani ya uchaguzi inaitaka serikali kusogeza huduma ya karibu na wananchi. Lengo ikiwa ni kuhakikisha huduma bora za maji safi na salama zinzpatikana kwa kuongeza Miundombinu ya maji. Aidha ujenzi wa miundombinu mikubwa ya maji katika makazi ya watumiaji nakuhakikisha Wananchi wanapunguziwa umbali wakufuata maji na kutekeleza Kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani. Miundombinu kadhaa imejengwa, mfano katika kata ya Kiseke tanki kubwa limejengwa kwa gharama ya **Tsh. 365,580,080.00** kwa fedha kutoka Serikali Kuu kupitia mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Mradihuu unahudumia wakazi **3600** wa maeneo ya Mlima wa Rada na Kiseke kwa ujumla.

### 7.1 Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwaka 2017 imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia Programu ya Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza, Miji ya Bukoba na Musoma, Miji Midogo ya Misungwi, Magu na Lamadi. Programu hii inajulikana kama "Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN)"

Kupitia Programu hii ya Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) inatekeleza na kusimamia miradi katika Jiji la Mwanza (Nyamagana na Ilemela), Miji Midogo ya Misungwi, Magu na Lamadi chini ya Ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank, EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Francaise de Developpment, AFD) kwa gharama ya **TZS. Billion 276.925 (Euro Milioni 104.5)**.

### 7.2 Mradi wa mradi wa ujenzi wa tanki la maji Buswelu.

Mradi huu umetekelezwa kwa lengo la kuboresha huduma ya maji kwa eneo la Buswelu pamoja na maeneo yanayozunguka tenki hili.
Mradi huu umekamilika na tenki limeshaanza kutoahuduma kwa baadhi ya wananchi. Mradi huu umegharimu jumla ya **TZS 5,106,000,000.00.**
Kazi zilizotekelezwa kwenye mradi huu ni :-

- Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa **lita 3,000,000.**

- Ulazaji wa bomba kuu la chuma 'steel pipe' lenye kipenyo cha **300mm** kutoka Sabasaba hadi kituo cha kusukuma maji Kiseke lenye urefu wa **mita 2, 670.**
- Ulazaji wa bomba kuu la chuma lenye kipenyo cha 300mm kutoka kituo cha kusukuma maji cha Kiseke mpaka kwenye tenki kwa urefu wa **mita 9,120,**
- Ulazaji wa bomba la usambazaji (bomba la plastiki) lenye kipenyo cha 160mm kwa urefu wa **mita 2490,**
- Ulazaji wa bomba la usambazaji (bomba la plastiki) lenye kipenyo cha **200 mm** kutoka kwenye tenki mpaka nyumba za NHC kwa urefu wa **mita 2, 250.**
- Ujenzi wa kituo cha kusukuma maji Kiseke ambapo pampu tatu zenye uwezo wa kusukuma **lita 150,000.**

Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa Kata za Buswelu, Kahama na Nyamuhongolo. Maeneo ambayo yameanza kunufaika kwa sasa ni Buswelu, Bujingwa, Buhila Buyombe na Mwashosha. Hata hivyo MWAUWASA imeidhinishiwa kupatiwa fedha na Wizara kwa ajili ya kuongeza mitandao ya usambazaji maji. Mradi huu utanufaisha zaidi ya wakazi **47,178.**

### 7.3 Mradi wa Usambazaji Maji Mlima wa Rada (Kiseke)

***Mradi umekamilika na tayari unatumika kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo;***

1. Ununuzi, uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji (Rising main) umbali wa **km 3.0**.
2. Ununuzi, uchimbaji na ulazaji wa bomba za usambazaji maji zenye urefu zenye kipenyo cha **160mm mita 150**, kipenyo cha **63mm** umbali wa mita 600 na kipenyo cha **50mm** umbali wa **mita 1500.**
3. Ujenzi wa chemba tatu (3) kwa ajili ya "valve"
4. Ujenzi wa tenki la kuhifadhia ya maji eneo la mlima wa Rada lenye ujazo wa **lita 150,000.**
5. Ununuzi na Usimikaji wa pampu yenye uwezo wa kusukuma **lita 75,000** kwa saa. **365,580,080.00** Mradi huu umekamilika ambapo jumla ya **wakazi 2,147** wamenufaika na mradi huu



## 7.4 Mradi wa Usambazaji maji Nyamuhongolo

Ununuzi, uchimbaji naulazaji wa bomba kuula usambazaji maji Usambazaji maji(Gravity main) lenye kipenyo cha **200mm** kwa urefu wa **mita 504** na kipenyo cha 160 mm kwa urefu wa wa **mita 3,384** Ununuzi, uchimbaji na ulazaji wa bombaza usambazaji maji zenye kipenyo cha **90mm** kwa urefu wa **mita 1500, 63 mm** kwa urefu wa **mita 1488** na kipenyo cha **50mm** kwa urefu wamita 1**650** Manunuzi na ufungajiwa valve za usambazaji maji yenye 315 KVA mradi umegharimu **Tsh 348,953,796.00** Mradi huu umekamilika ambapo jumla ya wakazi **39,600** wamenufaika na mradi huu.

### PICHA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI



**Tenki la Buswelu lenye ujazo wa lita 3,000,000**



**Tenki la Nyasaka lenye ujazo wa lita 1,200,000**




**Tenki la Mlima wa Rada lenye ujazo wa lita 150,000**



**Ufungaji wa pampu kwenye Kituo cha kusukuma maji –mlima wa Rada**



Ufungaji wa pampu kwenye kituo cha kusukuma maji cha Kiseke

## 7.5 KAZI MBALIMBALI ZILIZOFANYIKA KWA AJILI YA KUBORESHA HALI YA HUDUMA YA MAJI KWA MAENEO YA PEMBEZONI AMBAYO MWANZONI YALIKUWA YANAHUDUMIWA NA MANISPAA YA ILEMELA ( BUGOGWE, SANGABUYE, KAYENZE N.K)

| No. | KAZI ZINAZOFANYIKA | KAZI ZILIZOTEKELEZWA (MACHI 2021-MACHI 2023) | CHANGAMOTO | HATUA ZILIZOCHOKULIWA. |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uzalishaji | Tuna vituo viwili vya uzalishaji maji ambavyo viko katika maeneo ya Igombe na Kayenze. Vituo hivi vinahudumia maeneo ya Kata ya Kayenze, Sangabuye na Bugogwe<br>Uboresahi wa vituo hivi ili viendelee kuzalisha maji na kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa. | Kukatika kwa umeme kwenye vituo vya uzalishaji.<br>Changamoto ya low voltage (upungufu wa nishati ya umeme) kwenye kituo cha Kayenze.<br>Changamoto ya kiusanifu wa bomba linalotoa maji ziwani, ambalo limekuwa likileta hitilafu pindi kunapokuwa na upepo mkali ziwani. | MWAUWASA kwa kushirikiana na TANESCO tupo kwenye hatua za uboreshaji wa mfumo wa umeme kwenye eneo la Kayenze ikiwa ni pamoja na ufungaji wa Transforma.<br>Changamoto ya bomba la kuingiza maji kwenye kituo cha uzalishaji Igombe, tunaendelea na maboresho ya ili kuondokana na changamoto hii. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Usambazaji wa huduma ya maji. | Tumefanya maboresho mbalimbali kwa lengo la kusogeza huduma kwa wakazi ambapo katika kipindi hiki tumeweza kutekeleza kazi zifuatazo.<br>Tumelaza bomba za usambazaji kwenye eneo la Kayenze kwa urefu wa kilomita 7.5 ambapo tumeweza kuunganisha kaya 186 pamoja na uwekaji wa vituo 23 vya kuchotea maji.<br>Tumelaza bomba za usambazaji kwenye eneo la Sangabuye kwa urefu wa kilomita 20 ambapo tumeweza kuunganisha kaya 3 pamoja na uwekaji wa vituo16 vya kuchotea maji.<br>Tumelaza bomba za usambazaji kwenye eneo la Bugogwe kwa urefu wa kilomita 18 ambapo tumeweza kuunganisha wateja 220 uwekaji wa vituo 36 vya kuchotea maji. | Ufinyu wa mtandao wa bomba za maji ukilinganisha na maeneo husika umechangia utoaji wa huduma kupitia magati/ vituo vya kuchotea maji, pia kaya nyingi kushindwa kuunganishiwa huduma ya maji. | MWAUWASA imejipanga kutekeleza mradi wa kuongeza mtandao wa Majisafi utakao ambatana na uboreshaji wa huduma ya maji kwenye kata ya Kayenze na Bugogwa ambapo kwa sasa mradi huo upo kwenye hatua za kutafuta mkandarasi (Tendering)<br>MWAUWASA tunaendelea na h atua ya awali ya usanifu wa mradi mkubwa utakaohudumia kata ya Bugogwe, Shibula, Kahama na baadhi ya eneo la kata ya Buswelu ambao utajumuisha ujenzi wa chanzo kipya cha maji eneo la Kabangaja, ujenzi wa matenki na ujenzi wa bomba za usambazaji maji. |
| 3 | Kazi ya upanuzi wa miundombinu ya usambazaji. | MWAUWASA imejipanga kutekeleza miradi wa usambazaji maji, ambapo Wizara imetuahidi kutupatia fedha kwa awamu kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wananchi, katika bajeti hii Wizara ilitutengea Tshs. 405,000,000/- ambapo kwa sasa tumeshampata Mkandarasi ambaye ataanza kazi ya ujenzi wa mitandao ya bomba kwa zaidi km 8 katika maeneo ya Bugogwa, Shibula na Kayenze. | - | - |

## 8.0 SEKTA YA AFYA

Manispaa ya Ilemela ina Hospital moja, Vituo vya **afya 10** kati yake 6 ni binafsi 4 za serikali na zahanati 33 kati ya hizo 17 za serikali na 16 za binafsi, maternity home 4 za binafsi Ibara ya 83 ya ilani ya uchaguzi inaitaka serikali kuimarisha huduma za afyaya mama na mtoto na kuzitoa bila malipo ili kupunguza vifo vya akinamamamawajawazito na watoto kwa kujenga miundombinu ya afya karibu na jamii, Kujenga Zahanati katika mitaa. Jumla ya zahanati 3 mpya zimejengwa na zimekamilika na zinatoa huduma kwa wananchi. Zahanati hizo ni Lumala, Nyamadoke, na Masemele zenye thamani ya **Tsh. 300,000,000.00**

Utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu hiyo, mbali na matakwa ya ilani vilevile ilikuwa ni ahadi ya kuboresha mazingira katika vituo vya afya na Zahanati kwa kuimarisha miundombinu na kuanzisha maeneo mapya ya huduma kwa kadri ya uhitaji hususani katika kata za pembezoni na Kisiwa cha Bezi kata ya Kayenze. Katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Disemba 2022 Idara ya Afya haikuachwa nyuma kwani kazi nyingi nzuri zimefanyika kuanzia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya, na ujenzi wa Zahanati. Ambapo Kituo kimoja cha afya kimejengwa (Kayenze), Zahanati tatu zimekamilika ambazo ni Masemele, Lumala, na Nyamadoke.

### 8.1 Hospitali ya Wilaya

Hospitali ya Wilaya ya Ilemela imejengwa katika Kata ya Bugogwa Mtaa wa Isanzu, ujenzi ulianza Mwaka 2018 ambapo Serikali iliipatia halmashauri ya Manispaa kiasi cha Shilingi Bilioni moja na milioni Mia Tano **Tsh 1,500,000,000/=** Fedha iliyotumika kujenga majengo 7 yaliyokamilika kati ya majengo 22 yanayotakiwa kujengwa kwenye hospitali ya Wila**ya.** Majengo hayo ni Jengo la utawala, Jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Stoo ya dawa, Maabara, Jengo la vipimo vya Mionzi, Jengo la kufulia nguo (Laundry) na Jengo la Wazazi.

Katika bajeti ya 2021/2022 Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassan ilitupatia pesa taslimu **Milioni Mia Nane (800,000,000/=)** kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Kuhifadhia Maiti (mortuary), Wodi ya Wanawake, Wodi ya Wanaume, Jengo la Upasuaji, na Kichomea Taka. Mradi ulianza tarehe **12/03/2022** na kukamilika Mwezi wa Saba ambapo sasa ununuzi wa dawa na vifaa tiba unaendelea. Tunaishukuru Serikali ya awamu ya Sita chini Rais Shupavu Mhe. Samia Suluhu Hassan jumla ya **Tsh 2,300,000,00** zimekwisha tumika.





**Sehemu ya majengo ambayo yamekamilika katika Hospital ya wilaya ya Ilemela, ujenzi wa miundombinu bado unaendelea.**

Maelekezo ya ilani ya uchaguzi yalielekeza ujenzi wa hospital za wilaya. Manispaa ya Ilemela ilianza ujenzi wa Hospital ya wilaya,. Awamu ya sita chini ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan alianza ujenzi wa awamu ya pili wa hospitali ya halmashauri; lengo ikiwa ni kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa ngazi yawilaya ili kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika kwa wagonjwa. Lengo lingine ilikuwa ni kupunguza vifo vya mamana mtoto kwa kushughulikia Rufaa zinanotoka Zahanati na Vituo vya Afya kwa ukaribu. Majengo yaliyokamilika hadi sasa ni; *Jengo la utawala, Wagonjwa wa nje (OPD), Stoo ya dawa, Jengo la mionzi, Maabara, jengo la kufulia/usafi na jengo la wazazi.* Awamu ya pili ya ujenzi wa wodi ya wanaume na wodi ya wanawake na kichomea taka upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji, jengo la kuhifadhia maiti limekamilika. Ununuzi wa dawa na vifaa tiba unaendelea, na baadhi vimeanza kupokelewa kama inavyoonekana hapa.



Vitanda vya vipya vya hospital vilivyotolewa na serikali kuu




Mashine ya Usingizi (Univerisal anesthetic) ktk Hospital ya wilaya



**Mashine ya kufulia nguo za wagonjwa ktk Hospital ya wilaya**




**Mashine mpya ya mionzi (X – Ray) iliyopokelewa katika Hospital ya wilaya**



Mashine ya Utrasound (Univerisal anesthetic) ktk Hospital ya wilaya



Mashine mpya ya mionzi (X – Ray)  katika Hospital ya wilaya mtaa wa Isanzu

### 8.1.1 Kituo cha Afya cha Kayenze

Kituo cha Afya kayenze kimekamilika tangu **July 2022,** tayari kituo kinatoa huduma kwa wananchi. Kimegharimu kiasi cha **Tsh. 500,000,000.00** Fedha kutoka Serikali Kuu (Tozo za Miamala ya Simu). Kituo kimepokea fedha kwa awamu mbili tofauti. Kituo kilianza ujenzi tarehe 12.10.2021 baada ya kupokea Fedha milioni mia mbili na hamsini **(250,000,000.00)** kutoka Serikali kuu ukiwa ni mgawo wa tozo za simu. Ujenzi uliofanyika kwa awamu ya kwanza ilikuwa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Utawala, na Kichomea Taka. Awamu ya pili ya ujenzi ilianza baada ya Serikali kutoa kiasi kingine cha **Tsh. 250,000,000.00** tareh**e 28/03/202**2 kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Mwl. Elias Hassan Masala kutuongoza viongozi na wananchi katika zoezi la kuchimba misingi kwa ajili ya Jengo la Kufulia, Jengo la Wazazi na Upasuaji pamoja na Njia (walkways). Lengo la kujenga kituo cha afya katika kata ya Kayenze ili kupunguza umbali wa akina mama wajawazito kutembea umbali mrefu kutafuta huduma.



### 8.1.2 Zahanati ya Masemele

Ujenzi wa Zahanati ya Masemele ulianza mwaka 2019 kufuatia uamuzi wa serikali ya mtaa chini ya Mwenyekiti ndg Sukari. Baada ya ujenzi wa msingi ofisi ya mbunge ilipeleka **tofali 1,000** pamoja na **250,000.00** kwa ajili ya

motisha siku ya kuchimba msingi. Kwa sasa zahanati hii imekamilika **mwaka 2022** kufuatia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia kutoa milioni mia moja **(100,000,000.00)** kwa ajili ya ukamilishaji. Tunamshukuru sana **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.**



**Zahanati ya Masemele jengo la wagonjwa wa nje (OPD) ujenzi umekamilika na tayari jengo linatumika.**

### 8.1.3 Zahanati ya Lumala

Zahanati ya Lumala ipo mtaa wa Lumala Magharibi katika kata ya ilemela. Zahanati hii ilikamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi rasmii tarehe **8/4/2022** baada ya ufunguzi uliofanywa na mkuu wa mkoa wa Mwanza. Zahanati hii ilianzishwa na wananchi kupitia viongozi wao wakiongozwa na Diwani Ndg Wilbert Kilenzi na ofisi ya Mbunge kuahidi kutoa tofali mpaka ujenzi unakamilika nilichangia tofali 8,500 zenye thamani ya **8,500,000.00.** Tunamshukuru Mhe. Rais na Serikali ya awamu ya Sita kwa kutupatia fedha Shilingi milioni mia moja **(100,000,000.00)** kwa ajili ya ukamilishaji, tunawapongeza pia viongozi na wananchiwa Ilemela kwa michango na utashi wao.



**Zahanati ya Lumala ujenzi umekamilika na inatumika**

### 8.1.4 Zahanati ya Nyamadoke

Pia katika kipindi cha Nov. 2020 hadi Novemba 2022 tulifanikiwa kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Nyamadoke iliyopo kata ya Nyamhongolo ambapo pamoja na michango ya wananchi chini ya Diwani Cde. Anthony Nginila ofisi yangu pia ilichangia Tofali 7500 zenye thaman ya 7,500,000.00 na Mhe. Rais akatupatia shilingi Milioni mia Moja (100,000,000.00) kwa ajili ya ukamilishaji. Zahanati ilifunguliwa rasmii tarehe 08/04/2022 na wananchi wanafurahia huduma.

### 8.1.5 Zahanati ya Nyabusalu

Katika kipindi cha Nov 2020 hadi Novemba 2022 kwa kushirikiana na viongozi na wananchi wa kata ya Kiseke chini ya Diwani Mwevi Ramadhan Mwevi tulifanikiwa kuanzisha ujenzi wa Zahanati mpya ya Nyabusalu.Ujenzi bado unaendelea kwa ushirikiano wa Wananchi, Mbunge na Halmashauri ya manispaa ya Ilemela. Mchango wa mifuko 20 ya sementi yenye thamani ya **sh 400,000** litolewa na ofisi ya mbunge.

### 8.1.6 Zahanati ya Mihama

Ujenzi wa zahanati ya Mihama ulianza kufatia vikao vya mtaa wa Mihama kuona umuhimu wa kuwa na Zahanati kutokana na kuwa mbali na mjini na imezungukwa na shughuli za uvuvi ambapo magonjwa kama kichocho na malaria huwapata mara kwa mara. Mara baada ya wananchi kuanzisha ujenzi huu kwa kuchimba msingi na kununua mawe na kokoto ofisi ya Mbunge ilipeleka **mifuko 50** ya saruji yeny thamani ya **sh 1,000,000.** Ujenzi unaendelea kwa ufadhili wa TASAF. Tunawashukuru Tasaf kwa kuamua kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa zahanati ambayo itakapokamilika itahudumia wakazi wa Mitaa ya Mihama, Jiwe kuu





**Muonekano wa ndani, Nyumba ya mtumishi na Jengo la Zahanati ya Mihama Kata ya Kitangiri**



**Ujenzi wa Zahanati ya Nyambiti kata ya Buzuruga unaendelea**

## 9.0 HUDUMA ZA KIUCHUMI

### 9.1 Sekta ya Ardhi

Ibara ya 74 ya ilani ya uchaguzi inaitaka serikali, kukamilisha kupanga na kupima ardhi yote kwa kupima viwanja 66,000 hadi viwanja 79,000 Kuanzia 2020 hadi 2025. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa ardhi inapimwa, inapangwa na kumilikishwa kwa matumizi mbalimbali. Katika kutekeleza adhima hiyo, kupitia fedha za mkopo zilizotolewa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Manispaa ya Ilemela imekuwa mnufaika wa fedha hizo kati ya Halmashauri 58 zilizonufaika na mkopo huo nchini.

#### 9.1.1 Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (KKK)

Kupitia mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi, Manispaa imepima viwanja katika maeneo ya Buswelu, Nyafla, Sangabuye, Igalagala, na Ilekeko. Mradi umekamilika jumla ya **viwanja 3,254** vilimepimwa kwenye ekari 900 zilizopimwa, na umegharimu kiasi cha **Tsh. 3,589,774,000** Kutoka serikali kuu. Mpaka sasa Manispaa imefanikiwa kuuza viwanja katika mradi husika kwa asilimia 70% nakufanikiwa kurejesha mkopo wa Wizara kwa asilimia 100.

#### 9.1.2 Kuweka mazingira wezeshi kwaajili ya uwekezaji

Katika utekelezaji wa mradi wa KKK, Manispaa imefanikiwa kutenga maeneo 24 kwaajili ya kilimo cha mjini (Urban farming), Maeneo 13 kwaajili ya viwanda vidogo, Maeneo 30 kwaajili ya Hotel, Chuo eneo moja, Zahanati maeneo 3,Masoko maeneo 5, maeneo ya biashara zisizo rasmi 3.

Jumla ya hati **miliki 14,627** zimeandaliwa katika mazoezi yote ya urasimishaji, upimaji shirikishi na upimaji ujumla.

#### 9.1.3 Zoezi la urasimishaji makazi

Katika kipindi kinachotolewa taarifa Manispaa imefanya urasimishaji makazi ya wananchi mbalimbali kwenye maeneo ambayo hayakuwa yamepangwa na kupimwa na ambayo yalikuwa yanamilikiwa kimila. Jumla ya viwanja 8,614 vimepimwa katika mitaa 12 na kati ya hivyo viwanja vilivyomilikishwa ni viwanja 3,500.

#### 9.1.4 Uboreshaji Miji

Manispaa ya Ilemela iko katika mpango Kabambe wa Jiji la Mwanza. Katika suala la uendelezaji miji, Manispaa imeendelea kupanga na kuendeleza mji katika

Mitaa yake ambapo zaidi ya 80% mji umepangwa, Japokuwa kuna baadhi ya maeneo uendelezaji wake hauzingatii mpango kabambe wa Jiji la Mwanza uliopitishwa. Kutozingatiwa kwa masharti ya uendelezaji kunachangia kuwa na miji inayokuwa bila kupangika na hivyo kuharibu manthari ya mji.

### 9.1.5 Faida za upangaji miji na Upimaji Viwanja

Katika uboreshaji wa miji na Makazi ya wananchi, Manispaa ya Ilemela imeweza kupata faida zifuatazo;

(a) Usalama wa milki na makazi

(b) Miji inapangika na hivyo kupunguza kuwa na makazi holela

(c) Thamani ya ardhi inaongezeka

(d) Miradi inatumika kama chanzo cha mapato ya Halmashauri

(e) Kunakuwepo na uboreshaji wa miundombinu endelevu

(f) Kuongezeka kwa wigo wa makusanyo ya maduhuli ya serikali.



**Mkuu wa idara ya ardhi Ndugu Essau Mwakatumbula na timu yake akisikiliza na kero na kutoa elimu kwa wananchi wa Ilemela**



**Vijana wakiwa kazini tayari kwa kazi ya kupima viwanja katika eneo la mradi**



**Watumishi wa idara ya ardhi ilemela wakiwa uwandani kupima viwanja**

### 9.1.6 Utoaji wa hati miliki

**HATI ZILIZOWASILISHWA OFISI YA KAMISHNA WA ARDHI MKOA WA MWANZA NA KUKAMILIKA USAJILI WAKE KUANZIA DISEMBA 2020 HADI DISEMBA 2022**

| | Tar. 1 -31 Disemba 2020 | Januari 2021- Disemba 2021 | Januari 2022- Disemba 2022 | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|
| ILEMELA | 394 | 3422 | 3806 | **7622** |
| NYAMAGANA | 195 | 1296 | 2499 | **3990** |
| KWIMBA | 15 | 62 | 218 | **(295** |
| SENGEREMA | 26 | 208 | 165 | **399** |
| UKEREWE | 14 | 182 | 187 | **383** |
| BUCHOSA | 2 | 14 | 49 | **65** |
| MISUNGWI | 22 | 390 | 347 | **759** |
| MAGU | 63 | 306 | 415 | **784** |



**Timu ya msajiri wa hati mkoa wa Mwanza ikionozwa na Lenina Msajili msaidizi wa hati Mkoa akiwa na timu ya wataalam wa kugawa hati katika Kata ya Shibula manispaa ya Ilemela.**

## 10.0 SEKTA YA NISHATI

### 10.1 Huduma ya Nishati ya umeme wa REA maeneo ya Peri urban

Upatikanaji wa huduma ya umeme ndani ya Jimbo si mbaya sana ukilinganisha na mahitaji yaliyopo. Mpaka sasa upatikanaji wa meme mjini ni zaidi ya asilimia 90 wakati vijijini uko chini ya asilimia 30. Shirika la TANESCO limegawa wilaya ya Ilemela katika wilaya mbili za kihuduma Moja wilaya ya Ilemela na ya pili wilaya ya Nyakato. Adha huduma pia zimegawanyika katika makundi mawili, Umeme wa wa REA na umeme wa Tanesco. Huduma ya upatikanaji wa umeme katika wilaya ya Nyakato na Ilemela unatolewa kwa na kampuni mbili tafauti. Moja ni kampuni ya M/S NAMIS inayosambaza umeme katika maeneo ya pembezoni mwa mji yaani PERURBAN wilaya ya Ki-Tanesco Ilemela na umeme jazilizi kampuni ya SUGMCOM.

Katika kufanikisha usambazaji wa nishati ya umeme ndani ya jimbo la ilemela, kuna miradi mbalimbali ya usambazaji wa umeme iliyo chini ya mradi wa umeme vijijini (REA), katika kata ya Shibula, Bugogwa, Kayenze, Sangabuye, Kiseke na Buswelu. Aidha mradi wa ujazilizi unaendelea katika maeneo ya Iseni Kayenze 98%, Zenze na Buyombe 98%Kiseke, TX Mhonze Shibula, Kayenze ndogo Igombe 98%, Kayenze kubwa Kayenze. Idadi ya wateja waliounganishwa jumla ni 8,131(REA 1,245 na Tanesco 6,886).



## 11.0 HUDUMA ZA KIJAMII NJE YA MFUMO

Ofisi ya Mbunge imeendelea kushirikiana na jamii katika nyaja zote ikiwa ni kiuchumii, kisiasa, kijamii na utamaduni pasipo kujali itikadi za kisiasa nadini. Zifuatazo ni baadhi tu ya huduma za kijamii ambazo nimeshiriki kwa kipindi kifupi **toka Nov 2020** hadi **Disemba 2022.**

### 11.1 Gari kwa Ajili ya huduma kwa watumishi

Katika kipindi hiki kifupi ofisi ya mbunge ilifanikiwa kupata gari aina ya Mitsubish Delicia yenye thamani ya **shilingi milioni thelathini (30,000,000.00),** lengo likiwa ni kutumika kuwafikisha watumishi kazini hususani madaktari, manesi na watumishi wa kada nyingine za afya. Nia hii ilichagizwa hasa na ukweli kuwa hospitali yetu ya wilaya ipo mbali na hatuna makazi kwa ajili ya watumishi. Gari hilo lilikabidhiwa rasmi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya **Manispaa ya Ilemela tarehe 02.05.2022.**

### 11.2 Huduma kwaajili ya misiba

Gharama za kuhudumia misiba kwa kutumia gari la ofisi ya mbunge zimekuwa zikitofautiana kutokana na umbali ambapo kwa kata za Kayenze na Sangabuye kwa **mwaka 2020/2021** gharama zilikuwa ni **80,000.00 kwa trip** moja huku kwa kata kaza mjini gharama ikiwa ni **50,000.00** kwa trip.

Jedwali hapo chini linaonyesha idadi na gharama za misiba kwa kila kata kwa kipindi cha miezi kumi (10) kuanzia **January 2020** mpaka **July 2021** ambapo gari lilipata hitilafu na juhudi za kupata gari jingine zinaendelea kufanywa na ofisi ya Mbunge Kwa kipindi cha **miezi 25** jumla ya **sh 12,570,000.00** zilitumika kugharamia misiba mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao;January-December 2020 jumla ya **sh 6,270,000.00** zilitumika ukilinganisha na **sh 6,300,000.00** mwaka 2021/22 kama inavyoonesha katika majedwali hapa chini.

| Na | Mwezi | Idadi ya Misiba | Gharama ya kukodi Gari |
|---|---|---|---|
| 1 | Januari | 10 | 500,000/= |
| 2 | Februari | 09 | 460,000/= |
| 3 | March | 12 | 710,000/= |
| 4 | April | 10 | 550,000/= |
| 5 | May | 07 | 420,000/= |
| 6 | June | 11 | 560,000/= |
| 7 | July | 04 | 240,000/= |
| 8 | August | 14 | 700,000/= |
| 9 | September | 12 | 790,000/= |
| 10 | October | 05 | 350,000/= |
| 11 | November | 08 | 510,000/= |
| 12 | December | 08 | 480,000/= |
| | **JUMLA** | **110** | **6,270,000/=** |

| Na | Kata 2021 | Idadi ya misiba | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Kirumba | 1 | 40,000/= |
| 2 | Nyamhongolo | 2 | 160,000/= |
| 3 | Nyakato | 4 | 200,000/= |
| 4 | Mecco | 5 | 200,000/= |
| 5 | Nyamanoro | 1 | 40,000/= |
| 6 | Buzuruga | | |
| 7 | Bugogwa | 23 | 1,610,000/= |
| 8 | Ibungilo | | |
| 9 | Shibula | 15 | 900,000/= |
| 10 | Kayenze | 10 | 800,000/= |
| 11 | Nyasaka | 7 | 350,000/= |
| 12 | Buswelu | 3 | 180,000/= |
| 13 | Kahama | 6 | 360,000/= |
| 14 | Kiseke | 5 | 250,000/= |
| 15 | Sangabuye | 8 | 560,000/= |
| 16 | Ilemela | 3 | 150,000/= |
| 17 | Pasiansi | 1 | 50,000/= |
| 18 | Kawekamo | 7 | 350,000/= |
| 19 | Kitangiri | 4 | 160,000/= |
| **JUMLA** | | **103** | **6,300,000/=** |

## 11.3 Sadaka ya Iftari

Natambua kuwa katika siku za sikukuu mbalimbali, uhitaji wa jamii hasa watoto yatima wazee na wajane wamekuwa wahitaji wa huduma mbalimbali. Ofisi ya Mbunge imekuwa ikitoa misaada kwa makudi hayo mara kwa mara hasa nyakati za sikukuu. Sadaka hus就 iftar kwa makundi ya waislamu katika mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan katika kipindi cha mwaka 2021 na mwaka 2022 ambapo makundi ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira magumu, wajane na wazee wasiojiweza yalifikiwa. Aidha mwaka 2022 wanafunzi walio katika tasisi za elimu jimboni na nje ya jimbo, vituo vya watoto yatima, na makundi maalum katika jamii yalifikiwa. Yote hii ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na mfungo mwema lakini pia kujenga mahusiano katika jamii yetu ya wanailemela.

## 11.4 Ufadhili wa Elimu

Itakumbukwa kuwa katika kipindi cha 2015/2020 niliweka nguvu kubwa katika kusomesha watoto walioachishwa shule kwa changamoto za kupata ujauzito wakati wakiwa masomoni. Watoto hawa wa kike niliwachukua na kuwapeleka Chuo cha Malya ambapokila Kata kwa Kata 19 niliochukua watoto wawili kwa awamu ya Kwanza na awamu ya pili nilichukua watoto 93. Kati ya watoto 93 watoto 89 walihitimu vizuri kwa kutunukiwa vyeti vya kumaliza elumu ya sekondari na vyeti vya ufundi huku watoto 3 wakishindwa kuendelea na masomo kwa sababu ambazo hazijulikani.

Kwa kipindi cha Nov. 2020 hadi Disemba 2022, ofisi ya Mbunge iliendelea kutoa msaada wa kimasomo kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwa kadili nivyojaliwa katika suala la kifedha, ambapo jumla ya watoto watano (5) niliwapeleka Chuo cha Tandabui kwa ajili ya masomo ya Unesi, Famasia, Clinical Officers, na maendeleo ya jamii. Watoto hawa wanaendelea vizuri isipokuwa mmoja kutoka kata ya Bugogwa ambae kwa bahati mbaya alifukuzwa kwa kesi ya kukosa uaminifu katika chumba cha mtihani. Mtoto mmoja kutoka kata ya Bugogwa niliyeanza kumsaidia akiwa kidato cha tatu, badae kidato cha tano na sita kwa sasa yupo Chuo Kikuu cha Sayansi Mbeya (must). Ni matamanio yangu kuwasaidia wengi na nitaendelea kwa kadili hali itakavyokuwa ikiniruhusu.

## 11.5 Michango kwa Jeshi la Polisi

Lengo likiwa ni kuhakikisha Jeshi letu linatimiza majukumu yake ya ulinzi na usalama wa wananchi wa ilemela, nimeendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha baadhi ya changamoto zinafanyiwa kazi kwa haraka. Katika kipindi kifupi niliendelea kusaidiana na mkuu wa polisi katika ununuzi wa tairi 4 sh 1,600,000.00 na kuchangi tofali 2,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo vha Polisi kata na ukarabati wa gari la polisi, Futali kwa Askari waliokuwa wamefunga katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhan na ujenzi wa kituo cha polisi Kata ya Ilemela ujenzi ambao bado unaendelea. Jumla ya fedha sh 3,600,000.00 zilitumika kusaidia jeshi la polisi.

## 11.6 Serikali za Mitaa (ibara ya 122)

Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020/2025 katika ibara ya 122 inaielekeza Serikali katika kipindi cha miaka mitano kuhakikisha kuwa serikali za mitaa zinazidi kuboreshwa kwa lengo la kuinua ubora wa huduma kwa wananchi. Kwa kuzingatia uhitaji na utekelezaji wa Ilani kama ilivyoelekezwa katika Ibara 122(l), kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa katika kuhakikisha wanakuwa na mazingira bora ya kufanyia kazi, ofisi ya Mbunge ilitoa jumla ya tofali 12,600 zenye thamani ya shilingi 12,600,000.00 nakuzigawa katika mitaa mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za mitaa jimboni. Uboreshaji wa ofisi za serikali za mitaa utaendelea kufanyika hadi hapo mitaa yote 171 itakapo kuwa imekamilika kujengwa. Ujenzi wa ofisi hizi unafanyika kwa ushirikiano wa pande tatu kamba ambavyo kauli mbiu ya Jimbo inataka "Ilemela ni Yetu, Tushirikiane kuijenga" kwa maana ya Wananchi, Mbunge na Serikali., Mgao wa tofali tajwa hapo juu umefanyika kama ifuatavyo;



**Ujenzi wa Ofisi ya serikali ya Mtaa wa Nyamiswi kata ya Sangabuye ujenzi unaendelea**

**Ofisi za Mitaa zinazoendelea kujengwa na wananchi na mchango wa tofali wa ofisi ya mbunge**
**Kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini;**

| S/N | KATA | MTAA/KATA | IDADI YA TOFALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kiseke | Kabambo | 800 |
| 2 | Kiseke | Kiseke | 800 |
| 3 | Nyakato | Majengo mapya | 800 |
| 4 | Kahama | Kahama | 800 |
| 5 | Kahama | Isela | 800 |
| 6 | Kahama | Kadinda | 800 |
| 7 | Bugogwa | Bujingwa | 800 |
| 8 | Bugogwa | Kasamwa | 800 |
| 9 | Kayenze | Chasubi | 800 |
| 10 | Kayenze | Ihalalo | 800 |
| 11 | Shibula | Ilalila | 800 |
| 12 | Nyasaka | Kata | 3,000 |
| 13 | Ilemela | Ilemela | 800 |
| **JUMLA KUU:** | | | **12,600** |

Mgawo huu ni mwendelezo wa Utatu katika kutekeleza kauli mbiu ya Jimbo (Ilemela ni yetu,Tushirikiane kuijenga) ambapo wananchi huibua na kuanzisha mradi, Mbunge huchangia tofali na Mkurugenzi hukamilisha ujenzi wa mradi husika. Upande wa ofisi za mitaa katika awamu ya kwanza ya Ubunge tulifanikiwa kwa kushirikiana kujenga ofisi 11 kwa kushirikiana na wananchi, kati ya hizo ofisi 4 zimekamilika na zinatoa huduma kwa wananchi. Ofisi hizo ni;

Pia katika kipindi cha miezi 25 nimefanikiwa kuwakutanisha wenyeviti wa mitaa yote 171 na kuanzisha umoja wao ambapo ofisi ya Mbunge ilichangia gharama za chakula, posho ya nauli, shajara pamoja na ukumbi katika hoteli ya Monarch. Gharama ya kikao ilikuwa 4,642,000.00. Ofisi itaendelea kushirikiana na wenyeviti wa mitaa katika shughuri za maendeleo katika mitaa yao lengo ni kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa ngazi zote.



## 12.0 ZIARA NA MIKUTANO MBALIMBALI JIMBONI

Katika kipindi cha Nov 2020 hadi Octoba 2022 nilifanikiwa kufanya ziara tofauti tofauti 17 na mikutano 23 jimboni yenye lengo la kuwashukuru wananchi kwa kukipatia kura za ndio Chama cha Mapinduzi, kuwasikiliza, kutoa mrejesho wa bunge la bajeti na kutatua kero zao ambapo katika ziara zote ushiriki wa Chama , Serikali na ofisi ya Mbunge ulikuwa pamoja. Aidha wataalamu toka idara na taasisi zote za serikali walishiriki na kujibu hoja zilizojitokeza.

### 12.1 Ujenzi wa chama

Katika kipindi kinachotolewa taarifa, kama mwakilishi wa wananchi bungeni dhamana niliyopewa na Chama Cha Mapindunzi niliendelea kushirikiana kwa kila hali na viongozi wa wilaya kuhakikisha hakuna shughuli za chama zinazokwama ambapo michango mbalimbali ilitolewa kutegemeana na uhitaji ikiwa ni pamoja na **kufanya matengenezo ya gari la chama, kununua mafuta, shajara za ofisi, na gharama za vikao vya chama** ambapo jumla ya **Sh.28,306,900.00** ilitolewa kwa chama na jumuiya zake kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

## 12.2 Jedwali linaloonesha mgawanyo wa matumizi katika maeneo mbalimbali katika makundi mbalimbali.

| Na | Tarehe | Wahusika | Mratibu Mafunzo | Gharama |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 18.06.2022 | Wenyeviti wa Mitaa 171 yajimbo la Ilemela | Ofisi ya Mbunge &Mratibu waMkoa IlemelaSensa | 4,642,000 |
| 2 | 11.07.2022 | Viongozi wa Dini naTaasisi za Kidini | Ofisi ya Mbunge &Mratibu wa Mkoa& Kivulini Ilemela Sensa | 4,700,000 |
| 3. | 17.07.2022 | Wakina Mama Wajasiliamali | Ofisi ya Mbunge&Mratibu wa Mkoa & Kivulini Ilemela | 4,294,900 |
| 4. | 14.08.2022 | Baraza la Wazee laWilaya | Ofisi ya Mbunge&Mratibu wa Mkoa & Kivulini IlemelaSensa | 4,538,000 |
| 5. | 15.08.2022 | Jumuiya za Chama Map-induzi (W) Ilemela | Ofisi ya Mbunge & Mratibu wa Mkoa & Kivulini IlemelaSensa | 4,510,000 |
| 6. | 19.08.2022 | Halmashau-ri Kuu ya CCM(W) | Ofisi ya Mbunge & Mratibu wa Mkoa & Kivulini | 4,354,000 |
| 7 | | Vijana wahamasishaji wa sensa | Ununuzi wa tshirt 100 zenye mandishi ya ku- hamasisha sensa kwa ajili ya Viongozi | 1,268,000 |
| | **JUMLA KUU:** | | | **28,306,900** |

## 12.3 Michago ya mbunge kwa chama na jumuiya zake novemba 2020- disemba 2022

| NA | MAELEZO | CHAMA | UWT | WAZAZI | UVCCM |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa ofisi ya chama tawi la Lukobe na Ujenzi wa Ofisi ya Kata Kahama | 780,000/= | | | |
| 2 | Ununuzi wa viti 50 kwa ajili yavikao katika ukumbi mpya waofisi ya chama Buswelu | 882,500/= | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Ununuzi wa vitendea kazi, Laptop na Printer | | | 1,200,000/= | |
| 4 | Matengenezo ya gari la Chama | 2,400,400/= | | | |
| 5 | Gharama mikutano za vikao vya Chama na Jumuiya zake ngazi ya wilaya na mkoa | 7,150,000/= | 2,600,000/= | 1,450,000/= | 990,000/= |
| 6 | Zawadi za Kata 3 (Mecco, Kahama na Sangabuye) zilizo-fanya vizuri katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 | 1,800,000/= | | | |
| 7 | Ununuzi wa Sare za Chama Mkutano mkuu wa Jimbo, sare za Mabaraza ya Ju-muiya UWT, UVCCM na Wazazi | 18,000,000/= | 1,780,000/= | 1,500,000/= | 1,500,000/= |
| | Ununuzi wa sare za Vijana wa hamasa na Kombati za vijanawa UVCCM | | | 5,350,000/= | |
| 8 | Ununuzi wa bendera za chama | 2,000,000/= | | | |
| 9 | Ununuzi wa station- ary kwa ajili ya ofisi zote kuanzia tawi Mpaka wilaya na jumuiyazote | 8,700,000/= | | | |
| 10 | Ununuzi wa vifaa vyakujikinga na maam- bukizi ya corona 19 kwa ofisi zote kuan-zia ngazi ya matawi mpaka wilaya | 3,254,000/= | | | |
| | **JUMLA NDOGO** | **44,966,900/=** | **4,380,000/=** | **9,500,000/=** | **2,490,000/=** |
| | **JUMLA KUU** | | | | **61,336,900/=** |

## 13.0 SEKTA YA BARABARA

Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi kupitia shughuli za uzalishaji mali, ambao pia huchochea ongezeko la ajira.

**Mtandao wa barabara:** Wakala wa barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Jimbo la Ilemela wanahudumia mtandao wa barabara zenye jumla ya kilomita 875.85; Barabara za lami Km 37.16, Barabara ya zege Km 1.90, Barabara za udongo Km 740.596, Barabara ya Changarawe Km 91.53, Barabara za mawe Km 4.66, zinazojumuisha mtandao wa barabara zinazounganisha kata kwa kata, mtaa kwa mtaa na ambazo zinasimamiwa na TARURA. Aidha katika mtandao huo wa barabara, jumla ya Km 24.23 ni barabara zilizotokana na kufunguliwa upya na ofisi ya Mbunge, na tayari zimeingizwa kwenye mtandao wa barabara. Barabara hizo ni Barabara ya Igogwe - Sangabuye Km 8.73, Bujingwa **– Nsumba Km 2.5, Isela – Ng'wangwila Km 10 na Nyamhongolo – Majengo mapya.**

### 13.1 Mchango wa ofisi ya Mbunge katika matenenezo ya Barabara

Sekta ya barabara ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na jamii nzima kwa ujumla wake. Ofisi ya Mbunge imeendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya chama cha Mapinduzi katika kufungua barabara za **mtaa kwa mtaa** kujibu kiu na haja ya wananchi wa eneo husika, kwa kushirikiana na wenyeviti na wananchi wa mitaa husika. Katika kipindi kinachotolewa taarifa yaani, Novemba 2020 hadi Desemba 2022 jumla ya **kilomita 26.7** za barabara zimefunguliwa **katika mitaa 21, Jumla ya Sh 18,110,000.00** zimetumika katika mgawanyo ufuatao;

**wa mbunge Sh. 15,310,000.00 (Ukodishaji grader) na mchango wa Mchango wa wananchi Sh. 3,300,000.00 (Ununuzi wa mafuta na malipo ya operator)** na hivyo kufanya jumla ya **kilomita 75.4** ambazo ofisi ya Mbunge imefungua tangu 2016, na hivyo kurahisisha mawasiliano ndani ya Jimbo tofauti na ilivyokuwa awali.

**Barabara zilizofunguliwa Novemba 2020 hadi Desemba 2022;** Barabara ya Kabambo Kiseke Km 3.1, Barabara ya Nyasaka – Nsumba shule ya msingi Km 2.6, Barabara ya Bujingwa – Nsumba Km 1.8, Barabara ya Mwashosha Majarubani Km 1.9, Barabara za Mtaa wa Buteja Km 2.8, Barabara ya Buganda Km 2.3, Barabara ya Gedeli – Kangaye Km 2.2, Barabara ya Kaguhwa Buswekwa (Magu) Km 2, Barabara ya Iramba B – Bupumula Km 3, Barabara ya Nyamadoke – Majengo mapya Km 1.3, Barabara ya Zembwela
Busenga Km 2.2, Barabara ya Nyasaka – Nsumba Shule ya Msingi Km 2.1

# TAARIFA YA FEDHA YA BARABARA JIMBO LA ILEMELA

| BAJETI NAMAPOKEZI YA FEDHA KWA KAZI ZA UJENZI NA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA BARABARA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Na. | Jina la Mradi | Aina ya Barabara | | | | Madaraja/Maklavati | | Jumla | Fedha Zilizopelekwa Julai, 2022 – Machi, 2023 | Ute-kelezaji |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| | | Lami/ Mawe/ Zege | Tshs. | Changarawe (Km) | Tshs. | Mada-raja / Makalvati | Tshs. | Tshs. | Tshs. | Asilimia |
| | **TOZO 2022/2023** | | | | | | | | | |
| | Ujenzi (uongezaji wa tabaka la lami barabara ya Mecco (km 1.05) | 1.05 | 399,931,500.00 | | | | | 399,931,500.00 | 795,758,805.45 | 75 |
| | Ujenzi wa barabara ya Bigbite-Michungwani(km 0.7), na Mchongomani (km 0.1) kwa kiwango cha mawe | 0.80 | 496,959,073.00 | | | | | 496,959,073.00 | | |
| | Ujenzi wa barabara za mtaa Kirumba (Magomeni 0.6km, Kabuhoro - Ziwani (0.32km) kwa kiwango cha lami nzito (asphalt concrete) | 0.92 | 998,257,169.62 | | | | | 998,257,169.62 | | |
| | **JUMLA** | **2.77** | **1,895,147,742.62** | | **-** | **-** | | **1,895,147,742.62** | **795,758,805.45** | **75.00** |
| | **JIMBO 2022/2023** | | | | | | | | | |
| | Ujenzi wa madaraja ya Kahama – Isela-Ng'wamvilla, Butindo, ustawi na Tupendendane katika wilaya ya Ilemela | | | | | 4B | 179,335,660.00 | 179,335,660.00 | | |
| | Ujenzi wa barabara ya Nyarunduma (km0.78) na Nyamahoro – Msikitini (km 1.5) kwa kiwango cha changarawe; na ujenzi wa barabara ya Igombe - Ziwani (km 0.1) kwa kiwango cha zege katika wilaya ya Ilemela | 0.18 | 95,980,000.00 | 2.28 | 215,922,880.00 | | | 311,902,880.00 | | |
| | **JUMLA** | **0.18** | **95,980,000.00** | **2.28** | **215,922,880.00** | **4B** | **179,335.660.00** | **491,238,540.00** | **212,354,125.00** | **85** |
| | **MATENGENEZO 2022/2023** | | | | | | | | | |

# TAARIFA YA FEDHA YA BARABARA JIMBO LA ILEMELA

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Matengenezo ya kawaida (kuzibua mitaro na makalavati) katika barabara mbalimbali za wilaya ya Ilemela. | 21.04 | 11,030,366.00 | 66.44 | 348,316,334.00 | | 11,030,366.00 | | | | |
| | Matengenezo ya kawaida ( kuziba viraka) barabara za Bwiru, Kitangiri, Mecco, Furahisha, Pasiansi, Buzuruga, Penda, Tunza Loop na sanga – Kiloleli | 22.40 | 55,070,000.00 | | | | 55,070,000.00 | | | | |
| | Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Buzuruga- Mitimirefu- Makaburi (km 1.13), Mecco- TFDA (Km 0.87), Mecco – Majanini (km 0.85), Mwika (km 0.45)Nyamhongolo – Viwandani (km 1.7), Nyamadoke – Igoma – Mnadani ( Km0.78), Isela – Iwelyashinga Center (1.66km), Darajani Nyamhongolo – Kashsishi (km 0.06), Masemele – Ilalila Center (km4), sokoni – Bomani ( km1.5), Buswelu – Lukobe – Buyombe ( km 7), Mwaloni – Kigoto (Km 0.47), Bigbite – Michungwani (km 1.3), - igogwe – Kabusungu – Igumoyo – sangabuye Sec. (Km 8.73) na Kahama- Igombe ( km 9.12) | | | 39.62 | 472,080,745.00 | | | 164,639,926.00 | 809,452,413.03 | 97 | |
| | Matengenezo ya kipindi maalumu barabara za Nyamilolelwa – Bukala – Butindo – Ibaya – Ilalila (km 2.5) ,Igombe – Mahakamani (Km 0.7) , Ilemela – Mahakamani (Km 1.6) six (km 1.41) , barabara ya mawe Mkudi ( km 0.47) na Maduka tisa – uwanjani ( km 1.5) | | | 8.95 | 379,399,951.56 | | | | | | |
| | Matengenezo makubwa/ ujenzi wa madaraja ya Kagenzi na Iponya-bugali katika wilaya ya Ilemela. | | | | | 2B | 98,539,560.00 | | | | |
| | **JUMLA** | **43.44** | **66,100,366.00** | **115.01** | **1,199,797,030.56** | **2B** | **164,639,926.00** | **164,639,926.00** | **809,452,413.03** | **97** | |
| | **JUMLA KUU** | **46.39** | **2,057,228,108.62** | **117.29** | **1,415,719,910.56** | **6BC** | **343,975,586.00** | **2,551,026,208.62** | **1,817,565,343.48** | **85.67** | |

## 13.2 Baadhi ya Barabara zilizotengenezwa ni kama inavyoonekana hapa chini.



**Ujenzi wa barabara ya mawe Mkudi kata ya Nyasaka**



**Ujenzi wa barabara ya kabuhoro-ziwani kwa kiwango cha lami Kata ya Kitangiri/Kirumba**



**Ujenzi wa barabara ya Breweries (1km) kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh 499,953,596.20**



**Ujenzi wa mitaro barabara ya Pasiansi-Lumala-Kiseke Kata ya Kawekamo/ Ilemela/Kiseke**



Ujenzi wa daraja la Kilunguja Kata ya Kiseke na barabara ya Jiwe kuu kwa kiwango cha mawe Kata ya Kitangiri



Kuongeza tabaka la juu la lami kwenye barabara ya Mecco- Buzuruga (1.2km) gharama Sh. 399,931,500.00/=





**Matengenezo makubwa/ Ujenzi wa madaraja ya Kagenzi na Iponyabugali Kata ya Kayenze kwa gharama Sh. 98,539,560/=**



**UjenziwabarabarayaNyakurunduma(0.78KM)na barabaraya Nyamanoro - Msikitini (1.5KM) kwa kiwango cha changarawe**




**Ndugu Mpunzi Mbegeje mratibu wa shughuli za ujenzi wa miundo mbinu toka ofisi ya bunge wa Ilemela**



Mapeme leo Wazir wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya makazi ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe Dkt.Angeline SL Mabula amefanya ziara katika kufanya ukaguzi wa barabara Bighbite - Michungwani yenye urefu wa 700 M



Ujenzi wa mitaro na kalvati barabara ya Nyamanoro-Msikitini Kata ya Ibungilo Ujenzi wa barabara ya Igombe-Ziwani kwa kiwango cha zege Kata ya Bugogwa



Ujenzi wa barabara ya Bigbite – Michungwani (1.3KM)

## 14.0 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Wilaya ya Ilemela kwa mujibu wa ramani yake zaidi ya 87% ya eneo ni maji ya ziwa Victoria na 23% tu ndiyo nchi kavu. Kwa muktadha uchumi wa wilaya umebebwa na sekta ya Uvuvi, Ilani ya uchaguzi inaitaka serikali kuhakikisha vijana wanajihusisha na shughuli za ujasiriamali kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kuongeza kipato. Vikundi viwili vya vijana vimesajiliwa na kupatika mkopo wa Halmashauri, vikundi hivyo ni;

1. CHAPAKAZI chenye wanachama 8 kilichosajiliwa na kupewa namba ya usajili IMC/CD/CBO/1256 pamoja
2. CATFISH chenye wanachama 5 kimesajiliwa na kupewa namba ya usajili IMC/CD/CBO/CSH/00344

Vikundi vyote viwili vilipewa mafunzo kabla ya kukopeshwa**Tsh. 91,598,000.00** na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ikiwa ni sehemu ya mikopo ya 10% ya mapato ya ndani. Vizimba walivyowekeza vinakadiliwa kubeba samaki wasiopungua **40,000.** Kutokana na mwamko wa vijana katika suala zima la ufugaji samaki kwa vizimba, vijana wengi wamejitokeza kutaka kufuga samaki, changamoto ni mitaji. Ufugaji unaendelea katika mtaa wa Igalagala Kata ya Sangabuye. Mradi huu wa ufugaji wa vizimba ulikaguliwa na Kiongozi wa mbio za mwenge **mwaka 2022,** ni kati ya miradi iliyokuwa imepewa

kipaumbele kwa vijana kujiunga. Aidha jumla **Sh 296,647,780.00** zimetumika kati yake **sh 114,148,780.00** fedha toka serikali kuu na sh 182,499,000.00 toka mapato ya ndani kwa mgawanyo ufuatao; Ukarabati wa Mwalo Kayenze **sh 45,225,176.00,** Ukarabati mwalo wa Kayenze ndogo **Sh 85,348,780.00** OC ya idara **sh 28,800,000.00,** Ukarabati wa miundombinu ya soko la samaki **Sh 43,600,000.00** na uendeshaji ofisi **Sh 47,301,000.00.** Aidha mafunzo ya ufugaji samaki kwa vyama vya ushirika 11 vyenye washirika 48 wamenufaika na mafunzo. Vikundi hivi vinategemea kupata vizimba vyenye thamani ya **sh 3,859,899,200.00**



**Mradi wa Vijana wa ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba Mtaa wa Igalagala, Kata ya Sangabuye.**

## 14.1 Ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupimia samaki

Mradi wa ujenzi wa mzani wa kisasa wa kupimia mazao ya samaki katika mwalo wa Kirumba umejengwa na umekamilika. Mradi huu umeongeza kupato kitokanacho na zao la samaki. unakamilika ilikuongeza mapato. Mradi umekamilika na tayari unafanyakazi. Mradi umegharimu kiasi cha **Tsh.360,190,383.00** hadi kukamilika. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la mapato ukilinganisha na ilivyokuwa awali. Kabla ya mizani kujengwa mapato ya siku yalikuwa **Sh. 43,000,000.00** kwa sasa mapato ni zaidi ya **Sh.120,000,000.00** ushuru unaotokana na mazao ya uvuvi kwa mwezi katika Mwalo wa Kirumba. Aidha ushuru kwa mazao ya samaki yanayopelekwa nje ya nchi ilikuwa kabla ya mizani zilikuwa zinakusanywa **Sh. 80,000,000.00** kwa mwezi kwa sasa ni zaidi ya **sh 400,000,000.00.**



**Mzani wa kupima Mazao ya Samaki Mwaloni - Kata ya Kirumba umekamilika na unatoa huduma.**

Lengo ikiwa ni kupunguza utegemezi wa kibajeti kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, ikiwemo kuibua vyanzo vipya vya mapato. Manispaa ya Ilemela ilimepewa kipaumbele sana katika suala la miradi ya kimkakati, lengo ikiwa ni kukuza uchumi wa nchi kupitia ujenzi wa miundombinu hususa ni miundombinu inayobeba miradi ya vielelezo inayo weza kutoa ajira kwa watu wengi, lakini pia uchangiaji wake katika pato la taifa ukizingatia Mkoa wa Mwanza ni hub ya nchi za maziwa makuu. Baadhi ya miradi ya kimkakati iliyotekelezwa au inayoendelea kutekelewa ni pamoja na ifuatayo;

### 14.2 Upanuzi wa uwanja wa ndege

Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza na Ujenzi wa jengo la wasafiri linaloendelea kujengwa, kukamilika kwa jengo la kuongozea ndege, pamoja na rada ya kuongozea ndege, kukamilika kwake kutaongeza ama kukuza uchumi wa taifa kwa kiasi kikubwa.

### 14.3Mradi wa uboreshaji miji na majiji

Kuanza kwa mradi wa uboreshaji Majiji ambapo Jimbo la Ilemela litakwenda kufaidika na ujenzi wa soko jipya, barabara za mzunguko katika soko zenye Km 2.9, Barabara ya mzunguko toka Buswelu – Nyamadoke – Nyamhongolo yenye Km 9.2 na barabara ya Buswelu, Busenga hadi Cokacola Km 3

## 15.0 SEKTA YA KILIMO

Katika kipindi cha mwaka 2020-2022 kitengo cha mifugo kimetekela majukumu yake utoaji wa huduma za mifugo katika Manispaa ya ilemela kama ilivyokuwa imepangwa. Huduma hizi zilihusisha utolewaji wa elimu ya ufugaji bora na wenye tija ambapo jumla ya wafugaji 3167 walipewa elimu hiyo, Pia tulitoa huduma za udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa kuchanja mifugo hiyo(Jumla ya mbwa 683 walipata chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa). Vivyo hivyo huduma za matibabu kwa mifugo iliyougua ilitolewa. Pia tulifanya kaguzi za maduka ya pembejeo za mifugo na vituo vinavyojihusisha na uzalishaji na uuzaji wa chakula cha mifugo. Vile vile tumeendelea Kutoa huduma ya Usafi na Ukaguzi wa nyama kwenye machinjio zetu ndogo za Manispaa za Kayenze na Bugogwa (Igombe) ili kuwahakikishia walaji wa nyama kupata nyama safi na salama.

Halmashauri ya manispaa ya ilemela ina kadiriwa kuwa na idadi ifuatayo ya mifugo,

Ng'ombe wa asili na kienyeji ni 16332, Mbuzi 3977, 653, punda 196,Nguruwe 1003, na kuku kisasa na asili 57340.

### 1.1 Utekelezaji wa shughuli

Kwa kipindi cha mwaka 2020-2022 shughuli zifuatazwo zimetekelezwa katika halmashauri ya manispaa ya ilemela: Elimu ya fugaji bora, Uthibiti wa magonjwa ya mifugo na matibabu. Pia ufatiliaji wa huduma za uogeshaji mifugo, na ukaguzi wa nyama katika machinjio zetu ndogo mbili.

### 1.1.1 Utolewaji wa Huduma za ugani

Kwa kutumia maafisa mifugo waliopo kwenye kata zetu Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imetoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji 3167 katika kipindi cha 2020-2022.Huduma hii imesaidia wafugaji kupata uelewa wa ufugaji bora na wenye tija, Huduma hii hutolewa pale maafisa wanapokuwa wametembelea mfugaji kwa matibabu au kwenye vikao vya wafugaji. **Jumla ya shilingi 1,240,000/=** ilitumika kutoka mapato ya ndani.

### 1.1.2 Huduma za udhibiti wa magonjwa.

Katika kuhakikisha afya za mifugo zinalidwa kwa kuboresha utoaji elimu, matibabu na kuendesha zoezi la uchanjaji mifugo. Kitengo cha mifugo kimefanikiwa kusimamia na kutoa huduma za matibabu na chanjo kwa mifugo kama inavyooneka kwenye jedwali namba 1 na 2:

### Jedwali 1: Idadi ya Mifugo Iliyochanjwa

| **Aina ya Mifugo** | **Idadi ya Mifugo iliyochanjwa dhidi ya Magonjwa yafuatayo.** | | | | | **Gharama** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kideri | Gumboro | Ndui | Anthrax/ BQ | Rabies | Jumla ya shilingi **2,498,000/=,**Ilitumika kwa ajili ya kulipa posho kwa maafisa na usafiri,Pesa hii ni kutoka serikali kuu **(O.C).** |
| Ng'ombe | | | | 250 | | |
| Mbuzi | | | | | | |
| Kondoo | | | | | | |
| Kuku | 186740 | 128560 | 86345 | | | |
| Mbwa | | | | | 683 | |
| Paka | | | | | 28 | |

### Jedwali 2: Idadi ya Mifugo iliyotibiwa dhidi ya magonjwa

| Aina ya Mfugo | Idadi ya Mifugo iliyochanjwa dhidi ya Magonjwa yafuatayo. | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Anaplasmosis | ECF | Babesiosis | Pneumonia | Minyoo | Coccidiosis | Heart water | Mafua |
| Ng'ombe | 364 | 204 | 73 | | 784 | | | |
| Mbuzi | | | | | 302 | | 68 | |
| Kondoo | | | | | 126 | | | 84 |
| Kuku | | | | | | | | 14360 |
| Mbwa | | | | | 439 | | | |
| Nguruwe | | | | | 287 | | | |

### 1.1.3 Huduma za uogeshaji mifugo

Huduma hii hutolewa na wafugaji wenyewe kwa kutumia pump za kuoshea mifugo, katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya michovyo 173,564, ilifanyika kwa ng'ombe, Mbuzi na kondoo na mbwa. Hakuna Gharama yoyote iliyotumika kwa kuwa mfugaji mwenyewe ndo ununua dawa na kuosha mifugo hiyo. Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuiwezesha Manispaa kufanya ama kutekeleza majukumu yetu, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zimesababisha kutokufikia wafugaji wengi. Moja ni ukosefu wa vifaa vya usafiri na uchache wa watumishi ama wataalamu wa kilimo imesababisha baadhi ya wataalam,kuhudumu zaidi ya kata moja jambo ambalo linapunguza tija kiutendaji.

## 16.0 Miradi ya kimkakati

Ibara ya 122 (h) na 18 (b) (iii) inaelekeza Serikali kubuni na kuibua miradi ya kimkakati ambayo itaboresha utoaji wa huduma katika mamlaka za serikali za mitaa na kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Katika kutekeleza takwa hilo la ilani ya uchaguzi Ofisi ya Mbunge ilihakikisha miradi yote ya kimkakati iliyokuwa ama imebuniwa au imepangwa inatekelezwa. Baadhi ya miradi hiyo ni kama inavyoonekana hapa chini.

### 16.1 Ujenzi wa kituo cha basi na Malori Nyamhongolo

Ofisi ya Mbunge baada ya kuwa na changamoto kadhaa juu ya utekelezaji wa mradi huu, ilihakikisha ujenzi wa stendi uliokuwa umebuniwa na wataalam wetu unatekelezwa na unakamilikaili na kuongeza mapato na kupunguza utegemezi. Mradi umekamilika kwa gharama ya Tsh.26,649,749,438.00 na tayari unafanya kazi kuanzia mwezi Septemba 2022.

Mradi una vyanzo vifuatavyo vya kukusanyia mapato; **Jengo la Abiria, Jengo la Biashara, Maegesho ya Malori**, na **Hostel** kwa ajili ya kulalawageni.




**Hafla ya uzinduzi wa kituo cha mabasi na malori cha nyamhongolo uliofanya na Makamu wa Rais Dkt Philipm I. Mpango, pempeni yake baashi ya viongozi walioshiriki**





**Muonekano wa Standi mpya ya Bus, Maegesho ya Malori na Hostel katika Kata ya Nyamhongolo.**

## 17.0 KAMPENI ZA CCM



**Mgombea ubunge Dkt Angeline S.L.Mabula na Kheri James Mkuu wa wilaya ya Mbulu kwasasa akininadi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya ubunge 2015**



**Mmoja wa wapenzi na wakerereketwa wa CCM akisakata rumba na mgombea wa CCM katika uchaguzi Mkuu 2020**




**Baadhi ya vijana wa hamasa wakiwa wameshika mabango ya mgombea ubunge wa CCM katika uchaguzi wa Octoba 2020**






**Comrade Kheri James aliyekuwa Mwenyekiti wa vijana taifa akinitambulisha kwa wananchi ziku ya uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu 2020**



Nikipokea cheti cha ushindi toka kwa msimamizi wa uchagu haonekani katika picha kabla yakuongea na waandishi wa habari



Mmoja ya mikutano ya hadhara mgombea ubunge Dkt Angeline S.L.Mabula akimwaga sera za chama cha Mapinduzi



## 18.0 MIKUTANO YA CCM TAIFA





Baadhi ya wabunge wa mkoa wa Mwanza tukiwa katika Mkutano mkuu wa CCM taifa ukumbi wa Jakaya Kikwete Dododma



Wajunbe wa NEC toka mkoa wa mwanza. Angeline Mabula na Elen Bogohe




Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Ilemela ndugu Yusuph Bujiku akiwa na mbunge wa Ilèmela Mhe. Dkt. Angeline S.I Mabula (Mb) kwenye mukutano wa CCM taifa

## 19.0 MIKUTANO YA KITAIFA



**Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania akimwapisha Dkt angeline S.L.Mabula kuwa Waziri wa ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi**



**Picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Mh Samia S. Hassan Rais wa Jamhuri ya muungano baada ya kuapishwa kuwa waziri wa ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 9.2.2022**



**Mhe Nape Moses Mnauye Mbunge wa Mtama na Waziri na Dkt Angeline S.L.Mabula Mbunge na waziri wakiwa tayani kuingia bungeni.**



**Maelezo ni Waziri wa ardhi Dkt Angeline Mabula akipata maelekezo kutoka kwa waziri mkuu Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa**



**Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Ardhi Dkt Angeline S.L.Mabula akitoa ufafanuzi wa jambo bungeni.**






**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuzindua mradi wa Nyumba 644 zilizojengwa na Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania TBA katika eneo la Magomeni Kota Mkoani Dar es Salaam leo tarehe 23 Machi, 2022.**



**Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Ardhi akitoa ufafanuzi wa jambo kwa Mhe Kassim M. Majalia waziri mkuu**



**Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Ardhi Mhe Dkt.Angeline SL Mabula Kazungu Safari Idebe katibu wa Mbunge na Godfrey Nzawa afisa wa tarafa**

## 20.0 SEKTA YA MICHEZO

Ibara 242©,(f), (I) ya Ilani ya Uchaguzi ya ccm ya 2020/2025 inaelekeza kuendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki shughuli za kimichezo kwa kuanzisha vilabu vya michezo. Ofisi ya Mbunge kwa kushirikiana na idara ya Michezo na utamaduni ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zimeshirikiana kuhamasisha na kusimamia shughuri za kimichezo katika michezo ya mpira wa Miguu kupitia Angeline Jimbo cup, mchezo wa Bao, mpira wa Pete, kufukuza kuu, Draft ambapo zawadi mbali mbali zilitolewa zenye thamani ya Sh. 55,798,000.00 ikiwa ni pamoja na gharama ya jezi na vifaa vya michezo kwa miaka miwili inayotolewa taarifa.

Ibara ya 242 (i) inaelekeza kubuni na kuanzisha mikakati ya kuwezesha vijana kushiriki katika michezo ili kuimarisha afya zao, kudumisha amani, umoja na upendo uzalendo na madili kwa taifa. Ofisi ya Mbunge imeendelea kubuni na kusimamia mashindano Angeline Mabula Jimbo Cup ndani ya Jimbo langu la uchaguzi. Mashindano yameendelea kuwa chombo bora cha kuwaunganisha vijana kutoka katika mitaa 171 ya wilaya ya ilemela yakiimarisha afya zao, kuwafanya wamoja, na wazalendo kwa Taifa lakini pia, michezo kuwa sehemu ajira kwa wenye vipaji.



**Afisa michezo wa Manispaa ya Ilemela Ndugu Bahati Sosho Kizito akizungumza na wanamichezo ikiwa ni maandalizi ya michezo ya UMITASHUMTA**



**Tunawekeza kwa vijana ili kukuza vipaji, katika picha ni vijana chipukizi katika mchezo wa mpira wa kikapu wilaya ya Ilemela**



**Vijana wadogo wakiandaliwa kuwa wachezaji wa mpira wa kikapu, wekeza kwa vijana ili kulea vipaji kwa baadae.**



**Programme maalum kwa vijana kwa ajili mafunzo ya mpira wa kikapu Jimbo la ilemela chini ya Afisa Michezo Ndugu Bahati Sosho Kizito.**



**Timu ya mpira Kata ya Ilemela washindi wa The Angeline Jimbo Cup 2022**



**Timu ya kata ya Buzuruga iliyoshiriki The Angeline Jimbo Cup 2022**



**Baadhi ya viongozi wa Chama na Serikali pamoja na Makatibu wenezi wa CCM ngazi ya Kata walioshiriki katika uhamasishaji wa timu katika kata zao.**



**Timu ya mpira wa miguu toka Kata ya Nyasaka walioshiriki mashindano ya The Angeline Jimbo Cup 2022**



**Mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L.Mabula (Mb) akiwa na viongozi wa michezo viongozi wa serikali ngazi ya mkoa katika ufunguzi wa mashindano ya The Angeline Jimbo Cup.**



Utambulisho wa zawadi za mashindano ya mpira mbali na fedha taslimu zitolewazo kwa washindi wa mashindano kila mwaka




Viongozi wa timu ya volunteer wakijerumani Estelle Brulhart, Jurgen Seitz na Mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L.Mabula wakitoa vifaa vya mchezo




**Baadhi ya viongozi wa vilab mbalimbali vya michezo walionufaika na msaada wa mipira toka kwa volunteer waliojenga miundombinu ya viwanja vya michezo Sabasaba.**



**Zawadi ya draft kwa washindi wa mchezo wa draft ngazi ya Jimbo wakikabidhiwa na Mh. Adam K. Malima Mkuu wa Mkoa aliyekuwa mgeni rasmi**



## 21.0 MATUMIZI YA MFUKO WA JIMBO

### 21.1 Fedha za mfuko wa Jimbo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tshs. 60,396,000/=

| NA | KATA | MRADI/SHUGHULI | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1. | KATA ZOTE | Ununuzi wa simenti mifuko 2000 kwa ajiliya mradi wa matofali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule za Sekondari. | 39,000,000.00 |
| 2. | KATA ZOTE | Kulipa deni la mradi wa matofali uliofungwa. | 1,500,000.00 |
| 3. | KISEKE | Kuchangia mradi wa maji katika Kata ya Kiseke. | 1,000,000.00 |
| 4. | BUSWELU | Kuweka miundombinu ya kuhifadhi majikatika Shule ya Sekondari Buswelu. | 2,000,000.00 |
| 5. | NYAKATO | Kuunganisha miundombinu ya maji katikaShule ya Msingi Kangae. | 1,000,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | SANGABUYE | Ukamilishaji wa Ofisi ya Mtaa wa Lwashi. | 2,000,000.00 |
| | | Ukamilishaji wa Ofisi ya Mtaa wa Imalang'ombe . | 2,000,000.000 |
| 7. | KIRUMBA | Ununuzi wa viti vya walimu katika Shuleya Sekondari Kirumba. | 3,000,000.00 |
| 8. | MECCO | Ununuzi wa viti vya walimu ka-tika Shuleya Sekondari Kangae. | 2,000,000.000 |
| 9. | KITANGIRI | Ununuzi wa viti vya walimu katika Shuleza Sekondari. | 2,000,000.000 |
| 10. | NYAMANORO | Ununuzi wa viti vya walimu katika Shuleza Sekondari. | 2,000,000.00 |
| | | **JUMLA** | **57,500,000.00** |
| | | **SALIO** | **2,896,000.00** |

## 21.2 Fedha za mfuko wa Jimbo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Tshs. 83,761,000.00

| | KATA | MRADI/SHUGHULI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| **1** | KATA ZOTE | Kuwezesha ununuzi wa simenti kwa ajili ya mradi wa matofali kwaajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari/Msingi | **27,021,000** | Mifuko 1,300 imenunuliwa ufyatuaji wa to-fali unaendelea |
| 2 | KATA ZOTE | Ukarabati wa barabara za mitaa katika kata mbalimbali zin-azotarajiwa kufanyiwa maten-genezo kwa kuanzia ni pamoja na:<br>1.Mihama- Zahanati<br>2.Bwiru Sekondary – Manarani<br>3.Nyafla – Igumamoyo<br>4.Nyamwilekelwa | **15,000,000** | Pesa zimepele-kwa ofisi ya TARURA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | BUSWELU | Ujenzi wa Matundu manne (4) ya vyoo Shule ya Msingi Buhyila ambayo ni shule mpya ina vyumba vya madarasa matatu | **4,400,000** | Matundu ya vyoo manne (4) yamejengwa ikiwa ni pamoja na nguvu za wananchi. |
| | | Kuvuta Maji Shule ya Sekondari Bujingwa | **500,000** | Iko katika hatua ya manunuzi |
| 4 | NYAKATO | Malalamiko ya wananchi kuhusu changamoto ya Maji katika mtaa wa Kangae | **4,000,000** | Vifaa kwa ajili ya kusambaza maji vimenunuliwa na vimepokelewa site |
| | | Kuweka Umeme shule mpya Kangae Shule ya Msingi | **400,000** | Suala liko hatua za manunuzi |
| | | Uendelezaji wa Ujenzi wa Wodi ya Wazazi Zahanati ya Nyakato | | Tofali 6,000 zimetolewa, ujenzi uko hatua ya msingi |
| 5 | NYAMHONGOLO | Maombi ya mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya kuinua boma kituo cha Polisi Nyamhongolo | **2,300,000** | Ujenzi wa kituo ulishaanza uko ngazi ya msingi sementi mifuko 100imekabidhiwa |
| 6 | KAHAMA | Umaliziaji wa Jengo la maabara Zahanati ya Kata ya Kahama | **5,580,000** | Ujenzi wa boma umekamilika, tunasubiri Mkurugenzi kukamilisha ujenzi. |
| 7 | KITANGIRI | Ujenzi wa Matundu mawili ya choo Shule ya Sekondari Mwinuko | | Tofali 1,574 zimetolewa katika ujenzi huo |
| | | Ujenzi wa barabara ya Zahanati ya Mihama | | Mchango wa mifuko 50 ya sementi ulitolewa |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Kitangiri Kati | **5,000,000** | Pesa imepelekwa kwenye akaunti ya Mtaa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8 | SHIBULA | Utengenezaji wa madawati 50 ya Shule mpya ya Msingi Shibula | **3,500,000** | Utengenezaji wa madawati umekamilika |
| | | Shibula Shule ya Msingi kuweka umeme | **320,000** | Kazi haijafanyika |
| 9 | NYASAKA | Uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi ya Serikali ya Mtaa Nyasaka 'A' | | Tofali |
| | | Ujenzi wa Shule ya Msingi Nyamuge | | Tofali 3,500 zimetolewa ujenzi haujaanza |
| 10 | IBUNGILO | Ujenzi wa Madarasa 2 Shule ya Msingi Kiloleli | | Tofali 2,000 zimetolewa jengo liko hatua ya boma |
| 11 | SANGABUYE | Ukamilishaji wa jengo la malezi ya watoto wadogo Imalang'ombe | **5,000,000** | Jengo limefikia hatua ya upauaji |
| 12 | PASIANSI | Mradi wa Ujenzi wa Zahanati mpya ya Bwiru tofali 5,000 zimepangwa kutolewa | | Jumla ya tofali 2,500 zimetolewa |
| 13 | BUZURUGA | Uendelezaji wa Zahanati ya mtaa wa Nyambiti | | Jumla ya tofali zote 3,000 zimetolewa |
| 14 | NYAMANORO | Ujenzi wa Ofisi ya Serikali ya Mtaa Kilimahewa 'A', | | Jumla ya tofali 700 na Saruji Mifuko 10 zimetolewa |
| 15 | BUGOGWA | Ujenzi wa Sekondari Mpya Kilabela | | Jumla ya tofali 8,000 zimetolewa |
| | | Kuweka umeme Igogwe Sekondari | **320,000** | Taratibu za kuvuta umeme zinaendelea |
| 16 | KISEKE | Uongozi wa kata uliomba Mradi wa ujenzi wa jengo Zahanati Kiseke | | Tofali 4,000 zimetolewa ujenzi haujaanza |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 17 | KAYENZE | Ukamilishaji wa Ofisi ya Mtaa wa Iponyabugali | **2,500,000** | Mradi umeka-milika |
| | | Ujenzi wa Ofisi Serikali za Mitaa za Lutongo na Iseni | | Tofali 1,600 zimetolewa ujenzi uko hat-ua ya msingi |
| | | Ukarabati wa Nyumba ya Mwalimu S/M Kayenze | **3,000,000** | Ukarabati un-aendelea |
| 18 | ILEMELA | Ujenzi wa Ofisi ya Serikali ya Mtaa Lumala Mashari-ki. | | Tofali 1,200 zimetolewa mradi uko ngazi ya boma |
| 19 | MABATINI | Ujenzi wa jengo la kinywa FFU Mabatini tunadumi-sha ujirani mwema na wilaya ya Nyamagana | | Tofali 3,000 zimetolewa kwenye taasisi |
| 20 | Uwezesha-ji Makundi Maalum | Ununuzi wa Pikipiki na kompyuta mpakato kwa ajili ya shughuli za ofisi ya chama cha wasanii wilaya ya Ilemela | | Suala liko hat-ua ya manunuzi |
| 21 | | Fedha ya Tahadhari | **5,000,000** | |
| | | **JUMLA KUU** | **83,761,000** | |

## 21.3 Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka miwili ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya awamu ya Sita, chini ya uongozi thabiti wa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Chief Hangaya) Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Kuanzisha na kufungua shule 5 mpya za Sekondari ambazo ni Buzuruga, Igogwe, Semba, Nyamhongolo na Lubuka. Pia, kufunguliwa kwa shule 2 mpya za msingi (Bujingwa na Buyombe)

2. Halmashauri imeweza kukamilisha na kufungua Zahanati 3 ambazo ni Lumala, Masemele, na Nyamadoke ili kutanua wigo wa utoaji huduma za afya. Aidha, katika kuboresha huduma ya mama na mtoto, Halmashauri imekamilisha majengo ya kujifungulia katika Zahanati ya Nyakato na Ilemela.
3. Halmashauri imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kayenze. Na majengo muhimu ya Hospitali ya Wilaya na huduma za wagonjwa wa nje zinatolewa.
4. Halmashauri kwa kushirikiana na ofisi ya Mbunge wamefyatua tofali 76,335 na kuzigawa katika taasisi za serikali kama vile mashuleni, Zahanati kama Lumala, Masemele na Nyamadoke.
5. Ujenzi wa barabara ya Kabuhoro - Ziwani Mji mwema (km 1) kwa kiwango cha lami umefanyika kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri.
6. Vikundi vya Vijana, Wanawake na watu wenye ulemavu vipatavyo 102 ambapo wanawake (108) vijana (31) na walemavu (7) vimepewa mikopo kwa ajili ya kuimarisha mitaji yao ambapo Jumla ya Tsh. 1,032,185,263.00 zimepelekwa kwenye vikundi kwa ajili ya kuinua na kuboresha shughuli zao za kiuchumi.
7. Ufaulu kwa kidato cha Sita umependa hadi kufikia 99.6% na kidato cha nne hadi kufikia 95% hivyo kwa nafasi ya pili kimkoa na kwa elimu msingi katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imepata ufaulu kwa 96. na kushika nafasi ya 2 Kimkoa na 6 Kitaifa katika



**Mbunge wa Ilemela na waziri wa Ardhi akipokea maelekezo kutoka kwa Mhe Rais baada ya kuniapisha pembeni ni aliyekuwa naibu waziri wizara ya ardhi Mh Ridhiwani kikwete**

jengo la kujifungulia katika zahanati ya Nyamwiholela na Ilemela

## 22.0 Shukurani

Kabla sijahitimisha taarifa yangu, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutukirimia afya njema ya roho na mwili na kutuwezesha kutekeleza ahadi na maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya chama cha Mapinduzi. Aidha namshukuru sana Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kunuamini kumsaidia katika sekta ya ardhi kama waziri mwenye dhamana.

Ninawashukuru pia Mhe Dkt Philip Isidory Mpango Makamu wa Rais, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Wabunge wenzangu kwa ushirikiano na ushauri mkubwa wanaonipa siku zote. Nakishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kugombea nafasi ya ubunge, nawashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Ilemela kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuwawakilisha Bungeni na bila kuwasahau Viongozi wa dini mbalimbali kwa ushauri na maombezi yao.

Aidha ninawashukuru Madiwani wote wakiongozwa na Mstahiki Meya Renetus Bahebe Mulunga, Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa kwa ngazi zote kwa ushirikiano wao katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya 2020 – 2025. Mwisho japo si kwa umuhimu familia yangu kwa ushirikiano mkubwa wanayonipa na kuniombea utendaji wenye hofu ya Mungu, nami naendelea kukiri wazi kuwa dhamana niliyopewa nitaendelea kuitumikia kwa umahiri

## “MWANAMKE NI NGUZO YA MAENDELEO YA TAIFA, KWA PAMOJA TUNAWEZA”

## #KAZI IENDELEE#

"Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako".
*Yoshua 1:7*



**Mhe. Hassan Masala**
Mkuu wa Wilaya ya Ilemela



**Eng. Modest Apolinary**
Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela



**Mhe. Dkt. Angeline S.L Mabula (Mb)**
Mbunge Wa Ilemela na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MNEC)